# MTINDO WA NYIMBO ZA WATOTO WA SHULE ZA CHEKECHEA

NA

PIUS M. MWANZA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

2007

Mwanza, Pius M.
*Mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za*
2008/322531

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

PIUS M. MWANZA

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi.

PROF. GEOFFREY K. KING'EI

NA

DKT. JACKTONE ONYANGO.

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mke wangu Lilian Katile Musyoka pamoja na watoto wangu Jackson Nzoka Musyoka, Jaquiline Ndunge Musyoka, Evanson Mwanza Musyoka, Evalyne Muthikwa Musyoka na Elizabeth Mbithe Musyoka kwa kunipa moyo kuendelea na elimu yangu.

# SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii ili kuendelea na elimu yangu. Ninatoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu Prof. King'ei na Dkt. Onyango kwa kuniongoza vizuri na mashauri mema nilipokuwa nikitayarisha kazi hii. Sitamwacha nyuma mwenyekiti wa idara ya Kiswahili Bw. Mugambi kwa usaidizi wake.

Shukrani zingine ziende kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kuchukuliwa kuendeleza masomo yangu hapa pamoja na kupata mazingira mazuri ya kielimu chuoni.

Vile vile natoa shukrani nyingi kwa mke wangu Bi. Lilian Katile Musyoka aliyenisaidia kwa kila hali kukamilisha masomo yangu. Sitawasahau watoto wangu Jackson, Jaquiline, Evans, Evalyne na Elizabeth kwa kunipa mazingira mazuri ya kielimu usiku na kutohisi mpweke.

Shukrani za mwisho zitawaendea waalimu wa shule sita nilizotumia kufanyia utafiti wangu:- Bi. Theresia Musyoka-Ngomeni, Bi Catherine Mbithi-Katine, Bi Kasafiri-Nguluni Country side, Bi. Mutuku-Kanzalu, Bi. Maria Kilonzo -St Angelas na Bi. Muema –Katwanyaa ambao kama si kwa ushirikiano wao singepata data ambayo nimeitumia katika kufanikisha kazi yangu. Pia, ninashukuru Mubena Computers and Stationers kwa kupiga chapa kazi yangu. Pia



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

ninawashukuru wanafunzi wenzangu: Wanyela, Wanjala, Mary, Nancy, Kinoti, Asiku, Danson na Mutegi kwa kunisaidia kwa kila hali kufanikisha kazi yangu. Mwisho, nasema asanteni nyote na hata wote wale ambao sikuweza kuwataja majina yao na Mungu awabariki.

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Adodee** : Kubakia nyuma, kusalia kusoma, polepole.

**Chekechea** : Watoto wadogo, aghalabu wenye umri usiozidi miaka mitano.

**Dhahiri** : Bila kuficha; bayana; waziwazi; kinagaubaga

**Dosari** : Hali ipunguzayo ukamilifu kwa kitu; kasoro, ila, walakini.

**Fadhili** : Toa msaada wakati wa haja au shida; fanya hisani; fanya wema.

**Falsafa** : Elimu ya asili; maana na sababu za mambo au vitu

**Hadhi** : Heshima; staha

**Itikadi** : Imani au mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa au kiuchumi

**Kipengele** : Jambo au wazo mojawapo katika mada inayojadiliwa; mkabala wa jambo au wazo.

**Kusanifisha** : Kuweka vigezo maalum vya kusawazisha vitu ili vipate ulinganifu fulani wa pamoja

**Kuufutika** : Hali ya kuongea jambo kwa kuficha lisieleweke kwa urahisi.

**Matini** : Kifungu cha habari kilichoandikwa

| | | |
|---|---|---|
| **Mizani** | : | Idadi ya silabi katika mstari wa shairi; utenzi au wimbo. |
| **Mtitimo** | : | Hali ya kutoa sauti yenye mngurumo wa ndani kwa ndani |
| **Nadharia** | : | Akili nzuri; busara |
| **Pevu** | : | -enye kukomaa au-enye kuiva |
| **Sadifu** | : | faa |
| **Sambamba** | : | Ubavu kwa ubavu na bila ya kugusana; kulingana |
| **Shutuma** | : | lawama |
| **Sifabia** | : | Sifa za kijumla za jambo au kitu |
| **Staha** | : | Heshima inayoambatana na haya au aibu yakutenda jambo lisilo zuri mbele ya watu wengine. |
| **Taharuki** | : | Hali ya kusubiri kujua kitachotokea baadaye |
| **Tajriba** | : | Uzoefu alionao mtu katika kutenda jambo |
| **Tanabahisha** | : | Fanya mtu awe mwangalifu kuhusu jambo fulani |
| **Tashihisi** | : | Usemi wenye kukipa kitu kisicho uhai sifa ya kitu chenye uhai k.m. 'mlango ukamkodolea macho mgeni'. |
| **Uchu** | : | Hali ya kutamani sana kitu; kiu |
| **Upekuzi** | : | Hali ya kupeleleza; uchunguzi au udabiri. |
| **Vibonzo** | : | Picha zinazochorwa aghalabu magazetini ambazo hueleza wazo kwa namna ya kuchekesha; katuni. |

**Vipera** : Tanzu au visehemu mbalimbali vya jambo fulani.

## IKISIRI

Tasnifu hii inajadili swala la mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Nyimbo kumi na tano za lugha ya Kikamba, pamoja na za Kiswahili, ziliteuliwa kutoka shule tano za chekechea. Nadharia iliyotumika ni ya uhakiki wa kimtindo ambayo imehusishwa kwa kiasi kikubwa na Coombes H. Mihimili ya nadharia hiyo ilitumika kama dira ya kuuongoza utafiti huu katika kuyafikia malengo yake. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kuvitambua vipengele vya mtindo vilivyotumika katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea na kuonyesha jinsi vilivyochangia katika uwasilishaji wa maudhui. Data iliyotumika katika utafiti huu ilikusanywa maktabani na nyanjani. Maktabani tulipitia vitabu, magazeti, majarida na tasnifu yaliyosaidia kuupa msingi utafiti huu, kinadharia na kimpangilio wa data. Nyanjani tulitumia mbinu ya mahojiano. Data iliyopatikana, ambayo ilikuwa ni pamoja na nyimbo, ilichanganuliwa kwa kusikilizwa, kunukuliwa na kufasiriwa. Vifaa tulivyotumia katika ukusanyaji data vilikuwa ni pamoja na kinasa sauti, hojaji, karatasi na kalamu. Tulitoa matokeo kupitia njia ya maelezo. Jedwali pia ilitumika kuongezea nguvu maelezo. Matokeo ya uchanganuzi wa data yalidhihirisha kwamba nyimbo hizi zaweza kutumiwa kufunzia lugha na maudhui kama ilivyo katika tanzu zingine za kifasihi. Mwisho, mapendekezo ya utafiti yalitolewa.

# YALIYOMO

**Ukurasa**

Mada ....................................................................i
Ungamo.................................................................. ii
Tabaruku...............................................................iii
Shukrani................................................................iv
Maelezo ya Istilahi...................................................vi
Ikisiri......................................................................ix
Yaliyomo..................................................................x

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**......................1

1.0 Usuli .......................................................................1
1.1 Swala la Utafiti........................................................3
1.2 Madhumuni ya Utafiti...............................................4
1.3 Nadharia Tete...........................................................5
1.4 Sababu za kuchagua Mada.......................................5
1.5 Upeo wa Utafiti........................................................8
1.6 Misingi ya Nadharia.................................................9
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada.................................13
1.8.0 Mbinu za ukusanyaji Data...................................17
1.8.1 Utafiti wa Maktabani...........................................17
1.8.2 Utafiti wa Nyanjani..............................................18
1.8.3 Mahojiano............................................................18
1.8.4 Mbinu za Uchanganuzi wa Data..........................19

## SURA YA PILI: HISTORIA NA MAENDELEO YA FASIHI YA WATOTONCHINI KENYA........................21

2.0 Utangulizi ...............................................21
2.1.0 Vipindi muhimu vya kihistoria Nchini Kenya.........21
2.1.1 Kipindi cha kabla ya Ukoloni...........................21
2.1.2 Kipindi cha Ukoloni.......................................25
2.1.3 Kipindi cha baada ya Uhuru............................31
2.1.4 Shida ya fasihi ya Watoto...............................37
Hitimisho.............................................. 38
2.2.0 Sifabia ya fasihi ya Watoto..............................39
2.2.1 Utangulizi.......................................................39
2.2.2 Fasihi ya Watoto..............................................39
2.2.3 Dhima ya Fasihi ya Watoto...........................41
2.2.4 Sifabia za fasihi ya Watoto.............................42
2.2.5 Uteuzi wa fasihi ya Watoto.............................47
Hitimisho.................................................48

## SURA YA TATU: MTINDO NA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA NYIMBO ZA WATOTO WA SHULE ZA CHEKECHEA........................................50

3.0 Utangulizi ...............................................50
3.1.0 Maudhui katika Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea...............................................51

3.1.1 Maudhui ya Elimu....................................51
3.1.2 Maudhui ya Umuhimu wa Mama kwa mtoto..........52
3.1.3 Maudhui Mengineyo.......................................53
3.2 Maelezo ya Sentensi kwa ujumla.........................54
3.2.0 Kiwango cha Sintaksia...................................54
3.2.1 Matumizi ya Sentensi Fupi Fupi.........................55
3.2.2 Matumizi ya Sentensi Ndefu Ndefu.....................56
3.2.3 Matumizi ya Sentensi zenye Muundo Huru...........57
3.3.0 Aina za Sentensi katika Nyimbo za Watoto
wa Shule Chekechea.......................................57
3.3.1 Sentensi Ndefu Ndefu......................................57
3.3.2 Sentensi Fupi Fupi..........................................59
3.3.3 Sentensi Tongole ..............................................62
3.4 Sentensi zilizobadilika Muundo wa Mpangilio
wa Maneno..................................................64
3.4.0 Jinsi Msamiati Ulivyoteuliwa...........................65
3.4.1 Utangulizi.......................................................65
3.4.2 Msamiati kwa jumla.........................................66
3.4.3.0 Uteuzi wa Msamiati Katika Nyimbo za Watoto
wa shule za Chekechea..................................69
3.4.3.1 Kuchanganya ndimi......................................69
3.4.3.2 Msamiati wa misimu......................................71
Tanbihi..........................................................73

**SURA YA NNE: MATUMIZI YA TAMATHALI ZA USEMI KATIKA NYIMBO ZA WATOTO WA SHULE ZA CHEKECHEA**.....................................73

4.0 Utangulizi ..........................................................................73

4.1 Maelezo ya Tamathali za Usemi...........................73

4.1.0 Uteuzi wa Tamathali za Usemi katika Nyimbo za watoto wa Shule za Chekechea..........................81

4.1.1 Matumizi ya Takriri...........................................81

4.1.2 Matumizi ya Misemo.........................................86

4.1.3 Matumizi Mengineyo ya Tamathali za Usemi..........89

Hitimisho...........................................................................90

**SURA YA TANO: HITIMISHO**.............................91

5.0 Utangulizi .........................................................................91

5.1 Eneo ya Kazi kwa Jumla.....................................91

5.2 Matatizo na Mafanikio Tuliokumbana Nayo...............97

5.3 Mapendekezo kwa utafiti zaidi...........................98

Marejeleo..........................................................................101

Kiambatanisho cha Kwanza.......................................107

Kiambatanisho cha Pili...........................................111



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli

Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutoa maudhui yake kwa lugha ya maneno ambayo hutamkwa au kutendwa. Kipengele cha lugha ni muhimu sana kwani ndicho kinachotofautisha fasihi simulizi na sanaa nyinginezo. King'ei na Kisovi (2005:7) wanaieleza fasihi simulizi kama sanaa ya mazungumzo ambayo ni ya kubuni na ambayo yanasimuliwa, kukaririwa, kuigizwa au kuhadithiwa. Sanaa hii huhusisha maingiliano ya kimawasiliano kati ya fanani au msanii na hadhira yake (Nandwa na Bekenya 1983:1). Maelezo haya ya maana ya fasihi simulizi pia yanaoana na yale ya Mazrui na Syambo (1992:2) wanaosisitiza kuwa fasihi simulizi ni sanaa ya matumizi ya lugha ya kubuni inayosambazwa kwa mdomo kwa njia ya kuimbwa, kughanwa, kuigizwa, kusimuliwa, kuumbwa, kufumba au kutegemea mafumbo na vitendawili.

P'Bitek (1973:20) katika kuongezea maana ya fasihi simulizi anasema inajumuisha tanzu zote za matumizi ya lugha ya kubuni zenye kutumia maneno kwa njia ya kitamathali au mafumbo ili kuwasilisha hisia za mwanadamu. Anaongezea kuwa kinyume na sanaa kama vile kujenga au kupaka rangi, fasihi simulizi hutegemea tu uwezo wa mwanadamu wa kutumia lugha. Kulingana na maelezo ya waandishi hawa, ni wazi kwamba kipengele cha lugha ni muhimu sana katika fasihi simulizi kwa sababu ndicho

humwezesha fanani (msanii wa fasihi simulizi) kuumba sanaa yake. Jambo la pili ni kwamba fasihi simulizi hubuniwa na kwamba husambazwa kupitia kwa mdomo. Kusambazwa kwake kwa mdomo kutoka mtu mmoja hadi mwingine au kizazi kimoja hadi kingine ndipo jina lake limetoka.

Vipera au tanzu za fasihi simulizi ni kama vile vitendawili, methali, nyimbo, hadithi, ushairi, misemo na kadhalika. Kazi itaitwa fasihi endapo tu itatazamwa kwa misingi ya kisanaa. Tanzu hizi zote zimetosheleza misingi hii ya kisanaa.

Nyimbo, kama tulivyoona hapo juu, ni mojawapo ya vipera vidogo vya ushairi simulizi katika fasihi simulizi. Nyimbo hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye wizani. Nyimbo pia ni tungo ambazo huwasilishwa kwa sauti kwa kuimbwa na aghalabu huwa na muundo wa kishairi.

Ili wimbo uweze kuvutia wasikilizaji, unahitaji kuwa na muundo maalum wenye uzito na lugha teule, ishara na picha nzito. Utafiti huu utachunguza kama nyimbo ambazo zinatafitiwa zimetosheleza mambo haya. Pia utachanganua mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea ili kuchunguza kama nyimbo hizi zinatosheleza kauli hizi.

Jamii imechukulia nyimbo za watoto kama nyimbo za kitoto zisizo na umuhimu wowote wa kufanyiwa utafiti.

Finnegan (1970:303) anasema:

> Inaelekea kwamba hakuna uhakika wa asasi yoyote inayoshughulikia nyimbo za watoto katika jamii nzima ya Afrika, jambo ambalo ni sawa na jamii ya Waingereza (Tafsiri yetu)

Kwa hivyo kuna haja ya kufanya utafiti huu ili kukosoa msimamo wa wengi kuhusu nyimbo za watoto.

**1.1 Swala la Utafiti**

Ni nadra sana kupata katika maisha ya kila siku ya jamii nyingi za Kiafrika shughuli ambazo hazikuandamana na nyimbo, ngoma au dansi. Nyimbo hizo zilitegemea aina ya sherehe na pia hadhira. Nyimbo zilizoimbwa katika matanga zilikuwa za huzuni, katika arusi, zilikuwa za furaha zenye kutoa mafunzo fulani kwa maarusi na wale waliohudhuria. Pia zile zilizoimbwa jandoni zilikuwa na mafunzo kwa wale waliopelekwa jandoni.

Watu wazima na vijana ndio waliohusishwa sana na nyimbo hizo. Watoto wa rika ya shule za chekechea hawakuhusishwa sana katika uimbaji wa nyimbo. Jamii iliwapuuza kwa ajili ya umri wao mdogo. Inaelekea msimamo huu wa jamii unaendelea mpaka leo kwa sababu hata sasa wengi hawajatafiti nyimbo hizi za watoto kwa undani. Zamani hizo hakukuwa na shule za kupeleka watoto na kwa hivyo wengi wanafikiri nyimbo hizi ni za kitoto ambazo hazina mtindo, maudhui wala lugha yenye kina au maana yoyote.

Ili nyimbo ziweze kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kwa watu wazima na hata watoto, ni lazima mtunzi atumie mtindo unaofaa. Utafiti huu umejihusisha na mtindo uliotumika katika nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea. Wambua (2001) akimnukuu Ilitsikaya (1976) anasema kuwa mtindo hauwezi kutenganishwa na maudhui, kwani kimoja husaidia kufanikiwa kwa chenziwe. Kwa hivyo, tunapochunguza mtindo bila shaka tutagusia maudhui katika kuonyesha namna mtindo ulivyofanikisha maudhui.

Katika utafiti huu, maswali yafuatayo yatajibiwa:-

i) Ni sifa zipi za kimtindo zinazodhihirika katika nyimbo hizi?

ii) Ni vipengele vipi vya kimaelezo na kimasimulizi vinavyopatikana katika nyimbo hizi?

iii) Nyimbo hizi zaweza kutumiwa kama hifadhi ya vipengee muhimu vya fasihi simulizi?

**1.2 Maudhumuni ya Utafiti**

Yafuatayo ni madhumuni ya utafiti huu:

(i) Kuvitambua vipengele vya mtindo vilivyotumika katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea na kuonyesha jinsi vilivyochangia katika uwasilishaji wa maudhui.

(ii)Kueleza mbinu za matumizi ya lugha katika nyimbo hizi na jinsi zinavyoweza kusaidia kuendeleza fasihi simulizi.

(iii)Kubainisha tamathali za usemi zilizotumiwa katika nyimbo hizi

### 1.3 Nadharia Tete

Katika utafiti wetu, nadharia tete zifuatazo zitatuongoza:

i) Mtindo uliotumika katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea umefanikisha kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

ii) Lugha iliyotumika katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea ni rahisi kueleweka.

iii) Waandishi wa nyimbo hizi hushurutishwa na hadhira yao kuteua lugha kwa njia maalum ili kuhakikisha kiwango cha juu cha uelewaji.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Ingawa fasihi simulizi imeshughulikiwa na wasomi wengi, vipengele vyake vingi havijatafitiwa; fasihi simulizi imepuuzwa, huku andishi ikisifiwa. Kupuuzwa kwa fasihi simulizi kunaifanya ipotee na kusahaulika.

Wamitila (2003:17) anasema kwamba fasihi simulizi ya Mwafrika ilitekeleza majukumu maalum katika maisha ya kila siku. Twatambua udhoofishaji na uporomokaji wa maadili kwa kizazi cha sasa kwa kukosa majukumu haya. Wamitila anaongeza kuwa fasihi simulizi, hasa tanzu za nyimbo, maghani, vitendawili, methali, hadithi na misemo zilisaidia kurithisha mila, historia yao, itikadi na utamaduni wao na mafunzo yenye maadili. Hapo nyuma tumesema kuwa watoto wa rika la shule za chekechea hawakushughulikiwa na jamii kupitia tanzu hizi. Enzi hizo

hawakupata huduma hizo za nyimbo. Hali hii ndiyo imetusukuma kufanya utafiti huu kuangalia kama tunaweza kufufua kazi hizi au majukumu yaliyotekelezwa na fasihi simulizi kupitia kwa nyimbo hasa kwa watoto waliopuuzwa na jamii.

Okhoba (1995) anasema kuwa mashairi ya watoto huwa ni njia ya kujiburudisha na kutosheleza mahitaji fulani ya kiakili. Kupitia mawazo yake, hata nyimbo hutekeleza kazi hiyo kwa watoto. Nyimbo hizi zaweza kuwa na maudhui na mtindo unaoweza kuchanganuliwa kinadharia kinyume na jamii.

Katika tafiti nyingi zilizofanywa, fasihi ya watoto, hasa upande wa nyimbo za watoto wa umri wa shule za chekechea, haijashughulikiwa kwa kiasi kikubwa mpaka sasa. Finnegan (1970) amefanya utafiti wa nyimbo za watoto wa Afrika kwa jumla kwa kiasi kidogo tu bila kuingilia undani wake. Waandishi wengine waliofanya utafiti wa nyimbo za watoto waliweza kuonyesha aina za nyimbo hizi bila kuziingilia kwa undani pia. Hali hii ndiyo imetupa msukumo wa kutaka kufanya utafiti juu ya nyimbo za watoto ili tuweze kuzifafanua upande wa mtindo.

Kuna tafiti kadha ambazo zimetangulia utafiti huu na ambazo zinalingana kwa kiasi fulani na utafiti huu. Mifano ya watafiti hawa ni: Chiuri (1984), Nkonge (1988), Ntarangwi (1990), King'ei (1992) na Wambua (2001). Watafiti hawa wamefanya utafiti wa

nyimbo za watu wazima. Wambua (2001) alitafiti mtindo katika nyimbo, huku wale wengine wakishughulikia maudhui zaidi kuliko mtindo. Kwa hivyo tumeonelea kuna haja ya kujihusisha na mtindo katika nyimbo za watoto hawa.

Kinyume na ilivyokuwa zamani, inaelekea kwamba siku hizi watoto wengi huerevuka wakiwa bado wadogo. Hali hii yatokana na mabadiliko ya maisha. Wameerevushwa na vipindi vingi vya runinga na sinema, jambo ambalo halikuweko zamani. Kwa hivyo yafaa tuwashughulikie katika utafiti wetu ili tuweze kuwashirikisha katika fasihi ipasavyo.

Vile vile kupitia kwa mfumo wetu wa elimu nchini Kenya, masomo ya watoto wa shule za chekechea yanashughulikiwa. Hili ni jambo ambalo halikuwa likifanyika hapo awali. Wameweza kushirikishwa katika mashindano ya kitaifa na kwa hivyo utafiti wahitajika kufanywa ili uimbaji wao uweze kuimarishwa zaidi. Utafiti katika mtindo wa nyimbo zao ndio utaweza kuziimarisha zaidi kwa kuwa mtindo ni muhimu katika wimbo wowote.

Jambo lingine ni kwamba nyimbo hizi zimeanza kusahaulika kwa sababu siku hizi waalimu wa shule za chekechea hutilia mkazo nyimbo za mashindano pekee na kupuuza za kawaida. Kwa vile tunafahamu kwamba somo hili ni la lazima katika mfumo wa elimu humu nchini, kuna haja ya kufafanua nyimbo hizi za watoto kinadharia. Twahitajika kuelewa kwamba nyimbo hizi zina falsafa

zinazofanana na zile za watu wazima. Kwa hivyo, ni muhimu kuchambua mtindo wa nyimbo hizi tukijua watafiti wengine watajitokeza kuangalia maudhui na mambo mengine.

Kwa hivyo, utafiti huu kama tafiti anzilishi utaziba pengo ambalo limeachwa na waandishi na watafiti wa hapo awali.

**1.5 Upeo wa utafiti**

Utafiti huu umeshughulikia mtindo katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Haukuwekewa mpaka wa kipindi cha wakati nyimbo hizi zilipoimbwa. Umeshughulikia nyimbo za Kiswahili na za Kikamba. Katika utafiti huu, nyimbo za lugha ya Kikamba zimetafsiriwa kwenda lugha ya Kiswahili bila kupoteza mtindo wake. Nyimbo kumi na tano zimechaguliwa ambazo zimesaidia kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Nyimbo hizi zimechanguliwa kupitia kwa sampuli iliyochanganuliwa kwa kuzingatia maudhui.

Utafiti huu umefanywa katika kata ya Matungulu, wilaya ya Machakos. Shule sita zimechaguliwa ambapo tatu ni za umma na tatu za kibinafsi. Nyimbo hizi hutungwa na waalimu wenyewe wa shule hizi za chekechea na huweza kubadilishana wanapokutana katika semina au warsha mbali mbali. Watoto wenyewe ndio huweza kuziimba nyimbo hizi wanapofunzwa na kuongozwa na waalimu wao. Lengo la utafiti huu ni kwa hao watoto walioziimba na jinsi walivyoziimba bila kuzingatia yule aliyezitunga. Hali hii



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

imetoa mwangaza wa upekee unaopatikana kwa watoto hawa wanapoimba.

Nyimbo zinazofaa utafiti huu zimeteuliwa baada ya kuzisikiliza zikiimbwa na watoto hawa. Zilihifadhiwa kupitia kinasa sauti na baadaye kuandikwa katika daftari.

Maudhui yameshughulikiwa pia kwa sababu mtindo hauwezi kuchanganuliwa bila maudhui.

### 1.6 Misingi ya Nadharia

Nadharia ni muhimu sana katika uchanganuzi wowote wa kazi za kisanaa. Mada ya utafiti ndio huongoza ni nadharia gani itakayotumika.

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Coombes (1953) ni mojawapo wa waanzilishi maarufu wa nadharia hii. Kwa mujibu wake, anasema kuwa mhakiki sharti azingatie vipengee vinavyofanya kazi fulani iwe ya kuvutia. Anasema kwamba lengo la mtindo ni uchunguzi wa lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu zilizotengwa kwa kazi fulani ya kijamii, kueleza sababu ya vipengee fulani kutumiwa na vingine kuachwa.

Kupitia kwa maelezo haya ya Coombes imeamuliwa nadharia hii ndiyo inafaa kuchanganua mtindo na matumizi ya lugha katika

nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Pia nadharia hii imetumika katika kuchanganua lugha ya kitamathali iliyotumika katika nyimbo hizi.

Mwasisi mwingine wa nadharia hii ni Leech (1969). Katika maelezo yake kuhusu nadharia hii, alisisitiza kuwa huwezi ukachanganua fasihi kwa undani bila kuzingatia matumizi ya lugha. Kama vile Wambua (2001) anavyosema, ni umuhimu huu wa lugha ambao Leech (1969) anautaja uliotusajiisha na kututia changamoto ya kufanya utafiti wetu.

Katika utafiti wetu, tumejaribu kuchanganua matumizi ya lugha na vile vile kuchunguza uteuzi wa maneno ya nyimbo hizi na kwamba msanii alikuwa na kusudi gani katika kutumia maneno fulani badala ya mengine.

Lodge (1988) anasema kuwa mtindo ni jinsi ya kujieleza, ule upekee wa mwandishi wa kueleza kisanaa mambo ya kawaida. Ndiyo sababu uteuzi wa tamathali za usemi na msamiati hutegemea mtindo wa msanii binafsi. Kulingana na maelezo ya mwandishi huyu ni wazi kwamba mtindo wa msanii mmoja utakuwa tofauti na wa mwingine. Ndiyo sababu tunaweza kufanya utafiti wa aina moja lakini kazi za waandishi mbali mbali.

Wambua (2001) akimnukuu Ngara (1981) anasema ameorodhesha mbinu tofauti ambazo huzingatiwa katika utafiti wa kimtindo na

ambazo huchukuliwa kama mihimili ya nadharia hii. Aina mbili za mitazamo iliyojadiliwa na Ngara (1981) ni ule wa kiisimu na ule wa kifasihi. Anasema kuwa mtazamo wa kiisimu unashirikisha vipengele vifuatavyo:

(i) Kiwango cha sarufi ambapo huchunguza aina ya sentensi na uhusiano kati ya maana na muundo.

(ii) Kiwango cha msamiati ambapo mtafiti hujishughulisha na uteuzi wa mbinu kama vile jazanda, tashbihi na istiari na maana zake.

(iii) Kiwango cha kifonolojia ambacho hushughulikia vina, mdundo na kihunzi cha maneno.

(iv) Kiwango cha maana ya matini ambacho hujihusisha na kiimbo cha sauti na kuwepo au kutokuwepo kwa urasmi katika wahusika wa mchezo wa kuigiza au kati ya mwandishi na msomaji.

(v) Kiwango cha maandishi ambapo mambo kama vile chapa, rangi, alama zilizochapishwa, uwakifishaji na aya hushughulikiwa, kwani yanachangia katika ujumi wa kazi na katika kumvutia msomaji wa kazi ya sanaa.

Ngara (1981) anaendelea kusema kuwa katika mtazamo wa kiisimu-amali vipengee ambavyo hutumiwa katika utafiti ni tamathali za usemi kama vile taswira, taashira, methali, istiara na zingine ambazo haziwezi kuchanganuliwa kiisimu.

Kwa kutumia mihimili hiyo iliyoorodheshwa na Ngara, tumeweza kuchanganua nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Viwango ambavyo havihusiki katika uchanganuzi wa kifasihi havitashughulikiwa katika utafiti huu, kama vile, kile cha fonolojia ambacho hutumika katika uchanganuzi wa ushairi na cha matini kinachotumiwa katika uchanganuzi wa mawasiliano na maandishi.

Nadharia nyingine ambayo ingetumiwa kama ingetosheleza mahitaji ya utafiti wetu ni ile ya umuundo. Umuundo ni mtazamo wa nadharia isimu inayozingatia lugha kama mfumo wenye muundo. Nadharia hii ya umuundo inahusishwa na wana-isimu wa shule ya Prague ambao walihusika na urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Wasomi hawa waliathiriwa na mawazo ya wahakiki wa kirasimu wa nchi za Zeshi (Slovakia). Umuundo pia unawekewa msingi labda katika mihimili na mawazo ya Ferdinand de Saussure pamoja na mawazo ya ki-fenomenolojia ya Edmund Hussell (Wamitila 2002).

Wanamuundo waliuchunguza muundo wa ndani wa kazi za kifasihi, na hasa za kishairi ambazo walishughulika nazo zaidi. Katika hatua za mwanzo, wahakiki kama Roman Jakobson walivutiwa na kiwango cha sauti katika ushairi naye Jan Mukorovsky alichunguza swala la mizani katika ushairi wa Ki-zeshi. Wahakiki hawa baadaye walichunguza sanaa wakiilinganisha na hali za kijamii au hali za kijamii pamoja na jinsi

kazi za kifasihi zinavyoashiria uhalisi uliopo nje ya uwanda wa lugha.

Dhana ya muundo wa lugha inaelezwa kupitia mahusiano ya vipashio na vipengele bainifu vya matumizi ya lugha. Nadharia hii ya umuundo inaeleza juu ya aina ya uhakiki ambao unachunguza kaida zilizopo katika uundaji wa kazi fulani. Kwa kiasi fulani kama vile imedhihirika, nadharia hii yahusiana na isimu. Mtazamo wa isimu kama mfumo au muundo unaathiri wahakiki wa kimuundo wanaoiona kazi ya fasihi kama muundo. Lengo la nadharia hii ni kuchanganua muundo wa lugha kisayansi kwa kuzingatia vipengele vinavyojenga lugha.

Kwa hivyo, tungehitajika kuchanganua viwango vya kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki, ikiwa nadharia hii itatumika katika utafiti huu. Kwa vile utafiti wetu si wa kiisimu, basi imebainika wazi nadharia hii ya umuundo haitatumika katika utafiti huu.

**1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada**

Nyimbo ni kipengele cha fasihi simulizi. Baadhi ya wasanii na waandishi wameshughulikia fasihi simulizi kwa kujikita katika tanzu mbali mbali kama vile methali, ushairi, nyimbo za asili, vitendawili na kadhalika. Hawa wasomi na waandishi wameegemea upande wa maudhui na ni wachache sana walioshughulikia fani ya lugha kwa jumla.

Kati ya hao, wale walioshughulikia utanzu wa nyimbo ni pamoja na Finnegan ( 1970), Kirumbi (1975) Akivaga na Odaga (1982), Nandwa na Bukenya (1983), Kieti na Coughlin (1990), Miruki (1994), Wamitila (2002).

Ni muhimu pia kutaja baadhi ya wale walioshughulika na utafiti wa watoto hata kama si upande wa nyimbo, kwa sababu tutapata usaidizi fulani kutoka kwao. Baadhi ya watafiti hawa ni kama vile Gituku (1990) aliyejihusisha na maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya. Okhoba (1995) aliyefanya utafiti wa ushairi simulizi wa watoto wa Abamarachi; Mpesha (1995) aliyetafiti fasihi ya watoto nchini Tanzania.

Licha ya vitabu hivi, waandishi na watafiti hawa, kuna tafiti mbalimbali zilizoshughulikia utanzu wa nyimbo. Chiuri (1884) alifanya utafiti wa kuchanganua jinsi Kamaru alivyotumia lugha kuendeleza muziki wake. Utafiti wake ulihusu uhakiki wa maudhui na fani katika nyimbo hizi za Joseph Kamaru. Tumeweza kufaidika katika utafiti wake kwa sababu kipengee cha lugha alichokishughulikia ndicho ambacho tumejihusisha nacho.

Nkonge (1988) alitafiti nyimbo za Joseph Kamaru. Pia katika utafiti wake alichunguza fani na maudhui katika nyimbo za Kamaru. Sehemu iliyojumuisha fani ya utafiti wake imetufaidi sana kwa sababu utafiti huu unashughulikia fani vile vile.

Ntarangwi (1990) ni mtafiti mwingine aliyefanya utafiti wa nyimbo. Alijihusisha na maudhui katika nyimbo za Ramadhani Ongola. Amefanya utafiti katika nyimbo za kisasa. Aliweza kujihusisha na maudhui katika nyimbo za Ramadhan Ongala. Aliweza kubainisha jinsi kazi ya fasihi simulizi inavyosaidia kupitisha maudhui ya utetezi yaliyojitokeza katika nyimbo za Ongala, pia, jinsi maudhui hayo yalivyokuwa na uhalisi katika jamii iliyolengwa watu wa Afrika Mashariki. Kazi hii ya Ntarangwi imesaidia kupata mwelekeo wa jinsi ya kuchunguza na kuchanganua maudhui mahali imelazimika kuyatafiti.

King'ei (1992) alifanya utafiti juu ya nyimbo za taarabu nchini Kenya kutoka 1963-1990. Alitafiti lugha, utamaduni na mawasiliano ambapo aliweza kuchunguza nafasi ya nyimbo za taarabu nchini Kenya kati ya miaka hiyo. Aliweza kuchanganua muundo wa nyimbo hizi za taarabu kama mbinu moja ya kuwasilisha hisia za kijamii na kitamaduni.

Vile vile alichunguza mtindo wa nyimbo hizo. Utafiti wake King'ei (1992) umefaa katika utafiti huu upande wa mtindo na matumizi ya lugha.

Mtafiti mwingine aliyefanya utafiti wa kusaidia huu ni Osore (1994). Osore (1994) alitafiti mtindo katika riwaya. Alihakiki riwaya za Suleiman Mohammed kiisimu. Alichunguza jinsi maudhui ya riwaya za Mohammed ambazo ni *Nyota ya Rehema* na

*Kiu* yanavyobainika kupitia viwango vya sintaksia, semantiki na isimu amali. Osore hakuegemea sana tamathali za usemi kwa kuwa aligusia tu taswira na methali. Sehemu ya tamathali za usemi katika utafiti wake Osore imefaa utafiti huu.

Kamau (1994) alifanya utafiti wake kuhusu fani ya Mohamed Said Abdala. Alidhamiria kutafiti ufundi uliotumiwa na Mohamed katika riwaya zake na jinsi alivyowasilisha ujumbe wake. Alionyesha baadhi ya tamathali za usemi zilizotumiwa na mwandishi kama vile methali, misemo, sitiari na kadhalika. Alionyesha jinsi matumizi ya lugha yalivyoweza kuathiriwa na maisha ya mwandishi, utunzi wake na tajriba yake. Utafiti wake Kamau umefaa kwa upande mmoja kwa kuwa utafiti huu unahusu matumizi ya lugha na tamathali za usemi katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Tofauti inaingia upande wa kazi anayoshughulikia kwa sababu utafiti wake ni juu ya riwaya, lakini utafiti huu unahusu nyimbo.

Wambua (2001) alifanya utafiti kuhusu mtindo katika nyimbo za Kakai Kilonzo pamoja na matumizi ya lugha na tamathali za usemi. Alionyesha jinsi Kakai Kilonzo alivyoteua maneno na mbinu alizotumia katika kuwasilisha maudhui yake. Utafiti wa Wambua umesaidia kuendeleza huu kwa sababu tumetafiti mtindo wa nyimbo pia. Utafiti wake utatofautiana na huu kwa sababu alishughulikia nyimbo za mwimbaji mmoja aliyekuwa mtu mzima kinyume na utafiti huu ambao ni wa watoto.

Mutwiri (2005) alitafiti nyiso za tohara za jamii ya Watigania kwa kuzingatia mitazamo kuhusu utendakazi wa nyimbo za kiasili. Alilenga kuonyesha umuhimu wa nyimbo za tohara yenyewe katika jamii ya Watigania; na kueleza ni kwa nini tamaduni hizi hazifi licha ya upinzani mkubwa. Utafiti wa Mutwiri na huu unalingana hivi kwamba zote zatafiti nyimbo. Tofauti ni kwamba mtindo ndio umetafitiwa katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea naye Mutwiri alitafiti nyimbo za kiasili.

Kupitia tafiti ambazo tumeorodhesha, kuna pengo ambalo watafiti hawa hawajaliziba. Utafiti huu umeweza kuliziba pengo hili kwa sababu mpaka sasa hakuna mmoja aliyefanya utafiti kuhusu nyimbo za watoto wa umri huu wa shule za chekechea.

**1.8 .0 Mbinu za Ukusanyaji Data**

Mbinu za ukusanyaji data zilizotumiwa ni za maktabani na nyanjani.

**1.8.1 Utafiti wa Maktabani**

Katika utafiti huu wa maktabani, maktaba za Chuo Kikuu cha Kenyatta, Chuo Kikuu cha Nairobi na maktaba nyingine hapa nchini Kenya zimetumiwa. Upekuaji wa nyaraka mbalimbali, kumbukumbu, vitabu, majarida na tasnifu ambazo zinafaa katika utafiti huu zimetumiwa. Kutokana na upekuzi na uchambuzi wa maandishi, habari muhimu zimepatikana zinazohusiana na mada hii kama vile nadharia ya uhakiki wa kimtindo. Pia, kupitia

upekuzi huu, maelezo zaidi ya yale yaliyofanywa na wasomi kuhusu mada hii ya nyimbo yamepatikana.

Maelezo zaidi juu ya vipengele tofauti vya mtindo kama majazi, takriri na methali yamepatikana pia.

### 1.8.2 Utafiti wa Nyanjani

Kwa vile ni machache yaliyoandikwa kuhusu fasihi na nyimbo za watoto wa shule za chekechea, mtafiti ilimbidi kwenda uwanjani kukusanya data, mtafiti alitembelea shule za chekechea katika eneo la Matungulu. Shule hizi ziliteuliwa kulingana na umaarufu wa uimbaji. Umaarufu wa shule hizi wa uimbaji uliamliwa kupitia jinsi shule hizi zimekuwa zikifanya katika mashindano; matokeo hayo yalipatikana katika ofisi za elimu za eneo. Jambo lingine lililozingatiwa katika kuchagua shule hizi ni kwamba, kuna zile ambazo zinasimamiwa na makanisa, zile ambazo ni za kiserikali na zile ambazo ni za kibinafsi. Kupitia kwa mitazamo hii, shule tatu za umma na tatu za kibinafsi zimeteuliwa.

Mtafiti alipanga na waalimu wa shule hizi siku za kukutana na watoto hawa ili kuwasikiliza. Nyimbo hizi zilirekodiwa katika muktadha halisi kwenye kanda za kunasa sauti kisha ziliandikwa daftarini pia.

### 1.8.3 Mahojiano

Nyanjani waalimu wa shule hizi walihojiwa. Nia ya kuwahoji ilikuwa ni kupata historia na asili ya nyimbo hizi. Pia, kulikuwa na



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

haja ya kupata tafsiri ya misemo na maneno kadha ambayo waliyatumia katika nyimbo zao. Walieleza jinsi wanapata nyimbo hizi na mbinu wanazotumia kufunza watoto hawa.

Nyimbo zote walizoimba kwa lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili zilikusanywa. Sababu ya kuchagua zile za Kikamba ni kwamba eneo ambalo mtafiti ametoka linatumia lugha hii kama lugha ya mama. Kwa hivyo, utafiti wa nyimbo za lugha ya Kikamba umeweza kuwakilisha lugha za mama zote, huku lugha ya Kiswahili ikiwakilisha taifa lote kwa jumla ili kujumlisha matokeo.

Ili kupata sampuli ya kuchanganua, nyimbo zilizopatikana ziliwekwa katika makundi kwa kuzingatia maudhui ya nyimbo hizo. Baada ya kufanya hivyo, jumla ya nyimbo kumi na sita zilichaguliwa ili kufanyia utafiti.

### 1.8.4 Mbinu za uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa kuhusu nyimbo ilirekodiwa na kuhifadhiwa katika kinasa sauti na kunakiliwa katika daftari kwa lugha ya Kikamba na Kiswahili. Kwa kufanya hivi, utafiti ulichunguza kila sentensi katika wimbo kivyake ili kuweza kuchanganua matumizi ya lugha yaliyomo. Mtindo uliotumika katika nyimbo hizi ulichanganuliwa. Pia uchanganuzi wa maana na matumizi ya tamathali za usemi zilizotumika ulifanywa, na mwisho maudhui pia yalichanganuliwa.

Katika uchanganuzi huu wa nyimbo hizi, uzingativu uliwekwa katika madhumuni, nadharia tete na nadharia zilizoteuliwa na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo.

# SURA YA PILI

# HISTORIA NA MAENDELEO YA FASIHI YA WATOTO NCHINI KENYA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii itashughulikia historia ya fasihi ya watoto nchini Kenya, pamoja na sifabia za fasihi ya watoto. Lengo lake katika utafiti huu ni kutoa mwangaza wa yale mtafiti anatarajia katika utafiti wake. Sura yenyewe itakuwa na sehemu mbili kuu: ya kwanza ikiwa ni historia ya fasihi ya watoto, na ya pili sifabia za fasihi ya watoto.

## 2.1.0 Vipindi muhimu vya Kihistoria Nchini Kenya

Kulingana na Odaga (1980), historia ya fasihi ya watoto nchini Kenya imegawanyika katika vipindi vitatu vikuu yaani:-

a) Kipindi cha kabla ya ukoloni.
b) Kipindi cha ukoloni.
c) Kipindi cha baada ya ukoloni.

Kama asemavyo Weche (2000), vipindi hivi vitatu vimechangia, kwa njia moja au nyingine, katika kukua na kuendelea kwa fasihi ya watoto nchini Kenya.

### 2.1.1. Kipindi cha Kabla ya Ukoloni

Fasihi ya kipindi hiki ilikuwa fasihi simulizi na ambayo ilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo kwani

haikuwahi kuandikwa. Fasihi simulizi ilitokana na tajriba za watu maishani walipokuwa wakihusiana na wanajamii wenzao na vile vile kuingiliana na mazingira yao. Kwa hivyo basi, fasihi hii ilisheheni falsafa ya maisha ya jamii husika na vile vile ikasheheni imani za kidini ambayo yote yalikuwa mambo yaliyorithishwa kwa watoto na vijana ilipoendelea kupita ( Odaga 1980:4).

Fasihi simulizi katika kipindi hiki ilitekeleza majukumu kadhaa katika jamii za Kiafrika na ambayo yalipitishwa haswa kwa watoto. Baadhi ya majukumu haya yalikuwa ni kule kuwafunza watoto kuhusu historia ya jamii yao, maadili, utamanduni wao, matibabu, sanaa ya kiufundi, jinsi ya kujiheshimu na kuwaheshimu wengine.

Kulingana na Odaga (1980) na Akoleit (1990) fasihi simulizi ya kipindi hiki ilikuwa na tanzu dhahiri. Tanzu zilikuwa kama vile;

**a) Hadithi Simulizi**

Hadithi hizi zilikuwa aidha zile za kubuni zilizosimulia historia fulani na zilizosimuliwa kuhusu watu mashuhuri waliowahi kuishi katika jamii husika. Hadithi zilizotambiwa watoto ziliwaburudisha, kuwafundisha jinsi ya kuongea hadharani, mbali na kuwafundisha kuwa wabunifu kwa kujaribu kuzitunga hadithi zao wenyewe; zaidi ya hayo, hadithi ziliwasaidia watoto kuuelewa ulimwengu wao. Majukumu mengine ya hadithi yalihusu kuwafundisha watoto jinsi ya kuishi vizuri na

wanajamii wengine kupitia maudhui kama vile ulafi, uchafu na athari zake. Yaliyokuwa maudhui ya kawaida sana katika hadithi hizi na ziliwapa watoto picha halisi ya jamii yao na filosofia yake.

**b) Methali, Misemo, Vitendawili na Vitanza ndimi**

Utanzu huu nao ulijaa ujuzi uliopitishwa kwa watoto. Vile vile, utanzu huu ulisaidia sana katika kukiinua kiwango cha lugha cha watoto na kukuza kipawa chao cha kuongea.

Vitanza ndimi na vitendawili kwa mfano zilitumiwa katika kule kupima na kufundisha watoto jinsi ya kufikiria kwa haraka mbali na kuwaburudisha na kupitisha wakati.

**c) Nyimbo**

Nyimbo ziliimbwa katika sherehe nyingi na zilizotofautiana kwani kulikuwa na nyimbo za watoto, vijana wa kike na kiume, wanawake na wanaume. Pia zilitofautiana katika jamii moja hadi nyingine; nyimbo ziliweza kuburudisha hadhira na washiriki na wakati ule ule kutoa mafunzo mbali mbali hasa kwa watoto.

**d)Maigizo**

Katika kipindi hiki maigizo nayo yalipatikana kwa wingi. Maigizo yenyewe yalihusu matukio ya kila siku maishani. Maigizo haya yalihusu michezo ya uwindaji, maigizo ya vita



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

vya kikabila na maigizo ya vichekesho. Watoto nao waliingiza hali ya maisha kama walivyoyaona haswa wakiathiriwa zaidi na mazingira ya nyumbani. Zaidi waliiga tabia na mienendo ya wazazi na wanajamii wengine.

Aina mbali mbali za fasihi simulizi ya wakati huu zilifanyika katika mahali na wakati maalum. Kwa mfano, hadithi zilitambiwa watoto na nyanya au babu wakati wa jioni wakisubiri chajio. Nyimbo na maigizo nazo zilifanyiwa nje ambako kulikuwa na uwanja maalum uliokuwa umetengwa, na zaidi zilifanyika jioni wakati wa mbalamwezi.

Kwa kifupi, kama asemavyo Akoleit (1990), fasihi simulizi ndiyo fasihi ya zamani zaidi barani Afrika na, kwa hivyo, ndiyo hakika aina ya fasihi ya watoto ambayo ni kongwe sana nchini Kenya. Anaendelea kusema kuwa fasihi simulizi ndiyo iliyokuwa kifaa cha kufundisha Wakenya wachanga kwa kuwapa elimu ya kitamanduni.

Kipindi hiki cha kwanza katika historia ya fasihi ya watoto kilifikia kikomo mnamo karne ya 19 wakati Wazungu walipofika barani Afrika na baadaye kuuleta ukoloni. Watoto wa rika la shule za chekechea hawakuzingatiwa sana kwa sababu mambo mengi yaliendelea usiku ambapo wengi walikuwa wamelala. Kwa hivyo, fasihi katika kiwango hiki miaka hiyo haikudhamiria sana watoto hawa.

### 2.1.2 Kipindi cha Ukoloni

Kipindi hiki kilishuhudia kuingia kwa fasihi ya kikoloni ambayo twaweza kuifafanua kama fasihi andishi iliyoandikwa na wakoloni na kuandikiwa Wazungu (Akoleit 1990).

Weche (2000) naye asema kuwa fasihi ya kikoloni ni fasihi iliyoandikwa na wakoloni ili isomwe na watu wa nyumbani kwao. Kwa hivyo, kama asemavyo Mpesha (1995), kipindi cha ukoloni kilileta mabadiliko ya kifasihi kutoka fasihi simulizi hadi fasihi andishi.

Wasomi wengi walioandika juu ya fasihi ya watoto nchini Kenya na Afrika Mashariki kwa jumla wanakubaliana kwa wingi kuwa fasihi ya kikoloni ilipoingia, ilidunisha fasihi ya Kiafrika na kuipuuza sana. Lengo kuu ya fasihi hii ilikuwa ni kudhihirisha kuwa Wazungu walikuwa bora zaidi kuliko Waafrika waliosawiriwa na fasihi ya kikoloni kama wapumbavu na waliokosa maendeleo.

Kuhusu haya, Weche (2000) anasema kuwa nia kuu ya fasihi ya kikoloni ilikuwa ni kuharibu sura ya mtu mweusi kwa kumchora kama aliyekosa maendeleo yoyote yale. Anaendelea kusema kuwa mafunzo haya potovu yaliingizwa katika fikira za watoto wa Kiafrika kule shuleni jambo ambalo liliwaathiri kwa muda mrefu sana.

Naye Akoleit (1990), anaongezea kuwa fasihi ya kikoloni ilikuwa na nia ya kumsawiri Mwafrika kama mjinga na aliyeishi kama mnyama ili Wazungu wapate sababu tosha ya kumfundisha na kumstaarabisha Mwafrika. Anaeleza vile vile kuwa fasihi ya kikoloni ilijaribu kuonyesha uwezo wa Mzungu juu ya Mwafrika na kuwafanya Wafrika wajihisi duni ili waweze kutawaliwa na kunyanyaswa kwa urahisi na wakoloni.

Odaga (1980) anaongezea kuwa nia nyingine ya fasihi ya kikoloni ilikuwa ni kuwashawishi Waafrika kuwa fasihi yao na utamanduni wao ulikuwa duni na kwa hivyo walifaa kujifundisha desturi na tamaduni za wazungu zilizochukuliwa kuwa bora na pevu kuliko zile za Kiafrika.

Watoto wa Kiafrika waliojiunga na shule zilizoanzishwa na wakoloni walifunzwa fasihi andishi ya Mzungu. Lugha ya kupitisha fasihi hii mwanzoni ilikuwa Kiingereza na ilihusu kusoma vitabu shuleni. Vitabu vilivyoletwa na Wazungu ili vitumiwe katika shule za Kiafrika vilikuwa vimerahisishwa na vilikuwa vile vilivyosomwa na watoto wa kizungu kule kwao na vikadhaniwa kuwa vingewaburudisha watoto wa Kiafrika. Kabla ya kipindi cha ukoloni kuanza rasmi, wazungu tayari walikuwa wamefika barani Afrika kama Wamishenari au watalii. Wazungu hawa bila shaka walikuta Waafrika wakiwa na fasihi simulizi. Baadhi ya hadithi hizi ziliweza kuchapishwa na kutumiwa katika shule za msingi. Kati ya vitabu hivi ni kama vile:-

a) *Swahili Tales as told by Natives of Zanzibar* (1889) chake Mwingereza Edward Steere.

b) *Prosa Und Poesie Der Suaheli* (1906) cha Mjerumani C. Velten.

c) *Anthologie der Suaheli-Litteratur* (1894) cha Mjerumani Buttner.

Baadaye ukoloni ulipoingia Wazungu waliandika vitabu wakiwa na nia ya kumsifu Mzungu na wakati ule kumdhalilisha Mwafrika. Hata ingawa vitabu hivi vingi viliandikiwa watu wazima, vingi viliwafikia watoto, hasa kule shuleni. Mifano mizuri ya vitabu hivi na ambavyo vingine vilikuwa tafsiri ya vile vya Kiingereza ni kama vile *Out of Africa* cha Karen Blixen, *The Flame Tree of Thika* cha Elspleth Huxley.

Vitabu vingine viliandikiwa watoto wa Kiafrika na misingi ya ngano za Kiafrika. Hivi vilikuwa kama vile *Animal Palaver, Jungle Doctor Stories, Bibi Msemi,* ambavyo kwa kweli vilipata usomaji mwingi kutoka kwa watoto.

Wazungu pia walifanya tafsiri nyingi za riwaya na tamthilia za Kiingereza na Kiarabu. Maandishi ya Wazungu yaliyopata kutafsiriwa na kusomwa na watoto wa Kiafrika ni kama vile *Mashimo ya Mfalme Suleiman* cha Rider Haggard, *Kisiwa Chenye Hazina* cha R.C Stevenshop, *Mashujaa* cha Charles Kingsley na *Safari za Guliva* cha Jonathan Swift. Vile vile hadithi za

Kiingereza zilitafsiriwa kama vile *Hadithi za Mjomba Remus* na *Hadithi za Esopo*. Kazi za Kiarabu kama vile *Alfu Lela-Ulela* nazo zilipata kutafsriwa.

Tamthilia nazo zilijidhihirisha shuleni katika enzi ya ukoloni na mwanzoni zilizofunzwa zilikuwa ni za William Shakespeare kama vile *Romeo and Juliet*, *Macbeth*. Kama tulivyoona hapo awali , fasihi ya kikoloni ilinuia kumdunisha Mwafrika na wakati huo kumtukuza Mzungu. Jambo hili basi ni dhahiri katika maudhui na wahusika waliopatikana katika baadhi ya vitabu vilivyoandikwa na Wazungu kwa watoto wa Kiafrika ili wavisome shuleni au vingine visomwe na watu wazima wa aila ya Kiafrika.

Katika kitabu *Bibi Msemi*, Mwafrika amechorwa kama kiumbe kichafu na kilichozungukwa na mazingira machafu. Naye mtoto mchanga wa Kiafrika katika kitabu hiki awakilishwa na mhusika Tumbili. Hakika usawiri huu mbaya wa wahusika wa Kiafrika kwa kweli ulifaulu katika kuwapotosha wasomaji wachanga wa Kiafrika na kuwafanya wajidharau sana.

Katika *Mashimo ya Mfalme Suleiman*, Gagula, ambaye ni mwanamke mkongwe Mwafrika, ameelezwa kama zimwi. Haggaard vile vile aonyesha Waafrika kama wakatili kupitia mfalme Twala ambaye huwaua raia wake wengi kwa makosa madogo madogo.

Mnamo mwaka 1930 chama cha *Inter-Territorial Swahili Committee* kiliundwa kikiwa na jukumu la kusanifisha na kukieneza Kiswahili kote Afrika Mashariki. Jukumu moja la chama hiki lilikuwa ni kutia watu moyo wa kubuni na kuandika hadithi na vitabu vya Kiswahili. Kutokana na haya, tungo za kienyeji katika maandishi ya hati za Kilatini zilitokea. Waandishi wapya walichipuka kama vile James Mbotela aliyeandika *Uhuru wa Watumwa* (1934).

Katika mwaka wa 1936, Graham Hyslop, Mzungu aliyejihusisha na uigizaji alifika Afrika Mashariki na kuunda kikundi cha wanajeshi waigizaji kilichoitwa *East African Entertainment and Propaganda Unit Force* mnamo mwaka 1944. Katika mwaka wa 1953, tamthilia ya Hyslop *Afadhali Mchawi* iliigizwa na wanafunzi wa Jeans School na ikachapishwa kama kitabu mnamo 1957, pamoja na tamthilia yake nyingine ya *Mgeni Karibu*.

Kufikia mwishoni mwa kipindi cha ukoloni, kulitokea waandishi wa Kiafrika ambao waliziandika kazi za fasihi na ambazo kwa kweli zililengwa kusomwa na watoto shuleni. Mifano ni kama vile *Lila na Fila* cha Kiimbila, *Hadithi za Bibi Maahira* (1968) cha Baalary na *Hadithi za Hazina binti Sultan* cha C.A Sharif.

Tamthilia nazo zilibuniwa na watoto wa shule na kuigiziwa wazazi na waalimu mwishoni mwa kila mwaka wa masomo. Baadaye, wanafunzi hawa walitokea kuwa waandishi bora wa tamthilia

ambazo pia zilisomwa na kuigizwa shuleni (Mazrui na Syambo 1992). Baadhi ya waandishi hawa na kazi zao ni kama vile: Henry Kuria- *Nakupenda Lakini* (1957) na Gerishon Ngugi- *Nimerogwa Nisiwe na Mpenzi* (1961)

Vile vile, katika kipindi cha ukoloni, kulikuwa na fasihi ya Kihindi hasa, kutoka Uarabuni na India (Mpesha 1995). Kwa mfano, Isabela Fremont aliandika *Our Friend Manis* (1959) alichokiandikia watoto wa umri wa miaka saba hadi nane. Vingine vilikuwa kame vile *Ali Baba na Majangili Arobaine, Hekaya za Abunuwasi na The Magic Ring and Other Stories from India*

Pia watoto walifundishwa mashairi mengi yaliyokuwa ya Kiingereza kama vile *Baa Baa Black Sheep* na *Hey Diddle Diddle*. Mpesha (1995) asema baadhi ya mashairi ya kikoloni yalifanyiwa mabadiliko baada ya watoto kujifunza, kwa mfano, kubadilisha majina ya wahusika na mahali ili kuyafanya yakubalike zaidi na watoto. Vile vile watoto walitungiwa mashairi ya Kiswahili kame vile *Utaweza Kazi Gani?* lake A. Longman na lililosisitiza umuhimu wa kusoma. Ubeti wa kwanza ulisema,

*Usipojua Kusoma*
*U mjinga, U mjinga,*
*Usipojua Kusoma*
*U mjinga mkubwa mno*
(Mpesha 1995:113)



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kwa kuhitimisha, ni wazi kuwa kazi za fasihi ya kikoloni zilijaribu kumdhalilisha Mwafrika, huku zikimtwaza mkoloni. Pia, fasihi kwa watoto wa Kiafrika wa rika la shule za chekechea ilipuuzwa kwa sababu ilikuwa ya wale waliojua kusoma na kuandika. Watoto hawa walishinda na mama zao kwa wakati mwingi. Tena kama ambavyo tumeona hapo juu, mkoloni alishughulikia mtoto Mwingereza kwa kiasi kikubwa kuliko Mwafrika.

**2.1.3 Kipindi cha Baada ya Uhuru**

Kama asemavyo Odaga (1980), fasihi ya kipindi hiki ilijaribu kujengua mafunzo yaliyotokana na fasihi ya kikoloni kuwa Mwafrika ni kiumbe duni.

Aidha, kulingana na Mpesha (1995), fasihi ya kipindi hiki ilijaribu pia kufafanua matazamio ya Waafrika baada ya uhuru na kuonyesha mtazamo wa Mwafrika katika elimu.

Weche (2000) naye asema kuwa fasihi ya watoto ya kipindi hiki iliandikwa na Waafrika wakijaribu kurudisha hadhi ya Mwafrika kupitia mtazamo wa Kiafrika. Fasihi hii pia, kama anavyoendelea kueleza, ililenga kumfunza mtoto wa Kiafrika maadili ya kijamii mbali mbali na kuburudisha.

Odaga (1980) asema kuwa, watoto wa kipindi hiki wamegawanyika katika makundi mawili; yaani wale wa mjini na

wale wa mashambani na wote wakihitaji fasihi nje na ndani ya shule.

Kulingana na Akoleit (1990), fasihi ya watoto ya kipindi hiki imegawanyika katika matapo matatu makuu;

a) Fasihi ya kikoloni ambayo bado iliendelea kuwepo sambamba na ile ya baada ya uhuru.

b) Fasihi ya watoto wa Kiafrika iliyoandikwa na waandishi wenye asili ya kigeni na ambayo imeshindwa kuonyesha picha kamili ya fasihi ya Kiafrika.

c) Fasihi ya watoto ya Kiafrika na ambayo imeandikwa na Waafrika wenyewe. Fasihi hii inatilia maanani zaidi maslahi ya mtoto wa Kiafrika na tajriba zake.

Punde tu baada ya uhuru, mataifa ya Afrika Mashariki Kenya, Uganda na Tanzania, yaliungana na kuunda Jumuiya ya Afrika Mashirika. Huduma nyingi katika nchi hizi zililetwa pamoja. Kwa mfano, mashariki ya uchapishaji kama vile East Africa Literature Bureau na East African Publishing House yaliundwa na yalisaidia sana katika kuchapisha na kusambaza vitabu katika mataifa haya matatu.

Kiswahili kilitumiwa kwa wingi nchini Kenya na Tanzania na, kwa hivyo, vitabu vingi vya watoto viliandikwa kwa Kiswahili. Kazi za Kiingereza nazo ziliendelea kutafsiriwa kwa Kiswahili.

Wachapishaji walipiga chapa vitabu vilivyolenga daraja zote za mfumo wa elimu na yalihimiza matumizi ya vitabu vya fasihi madarasani.

Waandishi wengi wa Kiafrika walichipuka na kuviandika vitabu mbali mbali vya fasihi ambavyo viliwalenga watoto. Kwa mfano, Anne Matindi aliandika *Jua na Upepo*, Ndung'u akaandika *Hadithi Zetu* (1967) kiliochokuwa na hadithi kama *Mjinga Mtambara* na *Hofu ya Mutua*. Naye Amir aliandika *Hadithi za Wahenga* ambacho kiliwalenga watoto wa shule za msingi.

Hadithi za kale zilitumiwa na waandishi wengi katika kuzibuni kazi za watoto. Mifano ya vitabu vilivyotokana na hadithi kama hizi ni kama vile *Hadithi za Mapokeo, Hadithi Njoo, Sungura Kisimani* na *Shukuruni za Simba*. Vitabu vingine vya hadithi vilikuwa kama vile *The Proud Ostrich* cha J.K. Njoroge na *Someni kwa Furaha 1-3* cha Nelson. Vitabu vya vitendawili na methali vilichapishwa kama vile *Vitendawili Vyetu* na *Swahili Sayings*.

Kati ya maandishi mengine yaliyotokea kuwa maarufu sana kwa watoto baada ya uhuru ni yale ya Barbara Kimenye katika sanjari ya vitabu vyake vya Moses. Barbara Kimenye alikusudia vitabu vyake visomwe na watoto wa Kidato cha Kwanza na cha Pili katika shule za sekondari, lakini pia ilitokea kuwa viliwavutia sana watoto wa shule za msingi, hasa madarasa ya juu.

Vitabu hivi hasa viliandikiwa watoto wa nchi ya Uganda lakini vilisambaa kote Afrika Mashariki na kwingineko. Kitabu cha kwanza katika sanjari hii kilikuwa *The Smugglers* kilichoandikwa mnamo mwaka wa 1962. Vitabu hivi vimejaa maelezo chungu nzima juu ya maisha ya vijana wa shule ya upili ya Mukibi yaliyojaa raha na mikasa mingi. Hakika maswala kama haya yaliwavutia sana watoto.

Hata hivyo, Akoleit (1990) adai kuwa, vitabu hivyo vya Kimenye siyo vizuri kwa watoto, kwani vinawapotosha kwa wingi na kwa hivyo vyafaa tu kutumika katika kuwatia watoto hamu ya kusoma. Baadaye watoto wafaa kuhimizwa wavisome vitabu ambavyo vinawapa maadili mema.

Katika kipindi hiki cha baada ya uhuru, fasihi ya watoto pia imekuwa ikiendelezwa kupitia tamasha za kitaifa za muziki na michezo ya kuigiza nchini Kenya. Tamasha hizi mbili huwapa watoto nchini Kenya fursa ya kuvikuza vipawa vyao katika uimbaji, uigizaji, utambaji hadithi pamoja na kuyakariri mashairi. Ni kupitia tamasha hizi ambapo watoto shuleni huweza kujifunza mengi kuhusiana na utamaduni wa jamii nyingi nchini Kenya.

Tamasha hizi hufadhiliwa na serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pia makampuni ya kibinafsi kama vile kampuni ya magazeti na Nation na kampuni ya sigara ya B.A.T. huhusika katika kuzifadhili tamasha hizi mbili. Balozi za kigeni

nchini kama vile ubalozi wa Ufaransa pia huandaa tamasha za michezo ya kuigiza kwa lugha ya kifaransa na ambazo huhusisha shule mbali mbali nchini Kenya, hasa zile za upili.

Makanisa nchini Kenya nayo hayajaachwa nyuma katika kukuza na kuindeleza fasihi ya watoto nchini Kenya. Watoto wengi nchini huhusika na uigizaji na uimbaji kupitia makanisa yao mbali mbali. Maigizo haya na nyimbo mara nyingi huhusu mafunzo ya Biblia na pia hulenga kuwafunza watoto kuwa waadilifu katika jamii. Makanisa mengine pia huandaa mashindano ya nyimbo na michezo ya kuigiza ambayo huwasaidia sana watoto katika kuvikuza vipawa vyao mbali na kujifunza mienendo bora. Hakika wasanii wengi maarufu nchini katika uigizaji na uimbaji hukiri kuwa waliuanza usanii wao kule kanisani wakiwa watoto.

Hivi karibuni fasihi ya watoto imepata mwamko mpya, kwanza kabisa waandishi wa fasihi ya watoto wameongezeka maradufu kama vile Pamela Ngugi, Ken Walibora, Ezekiel Alembi kati ya wengine ambao wamezidi kuviandika vitabu vya watoto kwa mfano hadithi fupi, michezo ya kuigiza, majarida ya watoto na mashairi.

Kwa upande mwingine, wachapishaji wanaoviandaa vitabu vya watoto wameongezeka. Hakika kampuni zingine kama vile Sasa Sema Publishers hujihusisha kikamilifu katika uchapishaji wa vitabu vya watoto pekee. Wachapishaji wengine wa vitabu vya

watoto ni pamoja na Longhorn na East African Educational Publishers.

Mashirika ya utangazaji nayo hayajaachwa nyuma katika harakati za kukuza na kuendeleza fasihi ya watoto nchini Kenya. Kwa mfano, shirika la utangazaji la K.B.C redio huleta hewani kipindi cha watoto kila Jumamosi asubuhi na vile vile runinga ya K.T.N huonyesha kipindi cha watoto kwa jina *Club Kiboko.* Runinga ya Family nayo huwa na kipindi cha watoto wa shule za upili kwa jina *Rock Solid.* Ni jambo la kutia moyo kuona kuwa mashirika mengi ya utangazaji yanatilia umuhimu maswala ya watoto pamoja na fasihi yao. Vipindi kama hivi huwapa watoto fursa ya kuzitalii tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile hadithi, vitendawili, vichekesho na nyimbo bali na kuwaburidisha, kuwafunza maadili mema na zaidi kuvikuza vipawa vyao.

Serikali nayo imejikakamua katika kuhakikisha kuwa fasihi ya watoto inasomwa katika shule za msingi na sekondari Shirika la kukuza mitaala la K.I.E. limehakikisha kuwa fasihi simulizi na tanzu zake zote zimerudishwa kwenye silabasi na kuwa zinatahiniwa kama masomo mengine. Shirika hili limehakikisha kuwa maswala ibuka kama vile haki za watoto, janga la UKIMWI, maswala ya kinjinsia yanafundishwa watoto, hasa kupitia vitabu vya fasihi ya watoto.

Vyuo vikuu na vile vile vyuo vya kuwaandaa waalimu nchini pia vimeshiriki pakubwa katika kukuza na kuendeleza fasihi ya watoto nchini. Wanafunzi wa ualimu wanafundishwa jinsi ya kuwafundisha watoto fasihi yao ili waweze kukabiliana na ulimwengu unaobadilika kwa haraka sana.

Kipindi hiki ndicho kimekuwa na mwamko mpya katika kuwashughulikia watoto wa rika la shule za chekechea hasa miaka ya hivi karibuni baada ya uhuru. Shule hizi zilipoanzishwa fasihi ya hawa watoto iliweza kuimarishwa. Pia serikali ilipohusisha shule hizi katika mitaala yake, imefanya fasihi hii iweze kuendelea. Tena, kupitia kwa kampuni za uchapishaji wa kazi za watoto kama tulivyoona hapo juu, wachapishaji wapya wanaoshughulikia kazi hizi wamejitokeza na hivyo basi fasihi hii imepanuka zaidi.

### 2.1.4 Shida ya Fasihi ya Watoto Leo

Ingawa fasihi ya watoto nchini Kenya imekuwa na ufanisi, hasa katika miaka ya hivi karibuni, bado fasihi hii imekumbwa na shida chungu nzima. Shida hizi lazima zitatuliwe ikiwa fasihi ya watoto nchini Kenya itatakiwa kupata ufanisi zaidi. Kati ya shida hizi ni kama vile:

a) Waandishi wengi na wachapishaji wanaendelea kupuuza uandishi na uchapishaji wa fasihi ya watoto, na badala yake, kuegemea kwenye uandishi na uchapishaji wa vitabu vya masomo mengine ambavyo vina mauzo zaidi.

b) Waandishi wengi chipukizi nchini Kenya hukumbwa na shida ya fedha na kwa hivyo kazi zao haziwafikii wasomaji. Aidha, kampuni nyingi za uchapishaji hupendelea kuchapisha kazi za waandishi mashuhuri pekee kwani vitabu vyao vitanunuliwa kwa upesi. Ikiwa hivi, waandishi chipukizi hupuuzwa na kazi zao nyingi hazipati kuchapishwa kamwe.

c) Kuna shida ya wazazi kukosa kuwanunulia watoto vitabu vya kusoma na vile vile wazazi huwaelekeza watoto wao kwenye njia zingine za kustarehe badala ya kuhimiza watoto kusoma vitabu vya kifasihi wakati wanapokuwa huru.

d) Usomaji nchini Kenya hufanywa na wanafunzi kwa nia kuu ya kufaulu mitihani na, kwa hivyo, wanafunzi wengi hupuuza vitabu vilivyo nje ya silabasi zao.

e) Teknolojia mpya kama vile runinga hutegemewa na watoto zaidi ya vitabu vya fasihi na, kwa hivyo, hawapati wakati wa kuvisoma vitabu vyao. Teknolojia hii pia ina athari mbaya kwa watoto, kwani vipindi vingi havina maadili na utamaduni wa Kiafrika.

f) Umaskini nchini Kenya pia umezidi na, kwa hivyo, siyo Wakenya wengi ambao kwa hakika wanaweza kuwanunulia watoto vitabu vya fasihi.

**Hitimisho**

Ni wazi kuwa ingawa kipindi cha kabla ya ukoloni na cha wakati wa ukoloni vilipuuza fasihi ya watoto wa rika la shule za



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

chekechea, kipindi cha mwisho ambacho ni cha uhuru ndicho kimeweza kuipa fasihi hii kipaumbele. Hakutakuwa na upuuzaji tena wa fasihi hii.

Hakika, hali ya fasihi ya watoto nchini Kenya inazidi kuimarika tukizingatia idadi kubwa ya waandishi wa fasihi hii, ongezeko la kampuni za uchapishaji zinazojihusisha na uchapishaji wa fasihi ya watoto na zaidi juhudi za seriakli za kuendeleza na kuimarisha fasihi hii nchini Kenya. Shule za hawa watoto zinazidi kuongezeka pia.

### 2.2.0 Sifabia za Fasihi ya watoto

#### 2.2.1 Utangulizi

Ili kujadili kwa uwazi sifabia za fasihi ya watoto, kwanza ni sharti tuelewe vipengele vifuatavyo:-

1. Maana ya fasihi ya watoto.
2. Dhima ya fasihi ya watoto.
3. Sifabia za fasihi ya watoto
4. Uteuzi wa fasihi ya watoto.

#### 2.2.2 Fasihi ya Watoto

Ni vigumu kueleza maana ya 'mtoto' kwani kumeibuka fasihi tofauti zinazoegemea mambo tofauti katika kufafanua dhana hii, baadhi ya mitazamo inaegemea umri, utamaduni, uchumi na sheria.

Kwa jinsi hii, imekuwa vigumu kutoa maelezo kamili na kubalifu kuhusu fasihi ya watoto.

Davies(1973) amedai kuwa kuna shida katika kutofautisha kati ya fasihi na fasihi ya watoto. Anasema, maudhui yanayopatikana ndani ya fasihi kama ville ulevi, wizi na bidii huwahusu vijana na wazee. Je, vijana wenye umri wa kati waliovunja ungo na kubaleghe wawekwe wapi? kwenye umri mkubwa au watoto?

Maoni ya Davies ni kweli kwani kazi yoyote ile ya fasihi kwa kiasi kikubwa huwafaidi vijana na wazee. Hivyo, ni vigumu kutofautisha hizi fasihi kwa mfano hadithi ya Ken Walibora *Ndoto ya Amerika* inaweza kusomwa na mtu yeyote akaifurahia na kujifunza jambo.

Mpesha (1995) anasema kuwa fasihi ya watoto katika jamii yoyote ile hulenga kuwafahamisha watoto kuhusu mambo mazuri na mabaya, hisia na matarajio ya jamii walimozaliwa na kukulia.

Falsafa, itikadi na mabadiliko ya sera katika jamii wanamokulia watoto hawa huathiri aina ya fasihi inayowafikia. Watoto sharti wajuzwe kuhusu matamanio ya jamii, umuhimu wa kushirikiana kazini, utiifu na magonjwa hatari kupitia kwa nyimbo, hadithi na hata michezo ya kuigiza.

### 2.2.3 Dhima ya Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ina viwango sawa na zile zingine kwani matarajio ya wasomaji au wapokezi, watoto kwa wazee, ni sawa.

Davies (1973) anadai kuwa fasihi ya watoto sharti itekeleze mambo yafuatayo:-

i) Ipanue upeo wa fikra ya mtoto kuhusu ulimwengu kwa mfano kupitia kwa mafunzo ya amali za jamii, mahusiano ya watu.

ii) Kukuza usomaji wa watoto kwa kuzisoma kazi tofauti za fasihi kama vile ngano, kushiriki katika nyimbo, vitendawili na mafumbo bila kusahau michezo ya kuigiza ambayo ni maarufu kwao.

iii) Kazi ya fasihi impe mtoto furaha au burudani kupitia kwa picha za jalada au zinazoandamana na maelezo katika vitabu vya fasihi. Mapambo ya uigizaji vile vile husisimua nadhari za watoto na kutaka kushiriki katika maigizo. Hali hii huwapa watoto motisha ya kutangamana na kazi za sanaa.

iv) Kukuza tajriba za watoto kwa kupitia mahusiano ya wahusika katika fasihi. Watoto hujitambulisha na wahusika hao na kuweza kupata fahamu mpya kutokana na yale yananayowakumba wahusika tofauti.

v) Kuibua fikra zitakazoongeza matendo ya watoto katika nyanja tofauti za kimaisha kama vile elimu, michezo na uimbaji.

vi) Kumwezesha mtoto kujifahamu yeye ni nani? Anahusiana vipi na wengine? Vile vile kujifurahia na kukubali dosari na ufanisi wake. Mtoto atajifahamu zaidi iwapo picha nzuri inajitokeza katika wahusika. Iwapo kuna wahusika duni katika fasihi, ni sharti wapate adabu ili kukuza wema katika jamii dhidi ya uovu.

vii) Kukuza matumizi ya lugha. Mtoto anaposoma hadithi, kushiriki katika maigizo au kutazama vipindi vya vibonzo katika runinga, hujifunza msamiati mpya na kuweza kuutumia katika mawasiliano ya kila siku.

Shabaha hizi zote za fasihi ya watoto huazimia katika kumfanya mtoto kuingiliana vyema na wanajamii wengine. Pamoja na hayo, huweza kumfanya mtoto kuzijua zile amali na kuzitukuza hivyo basi akipata msingi bora wa kuwa na sifa kamili za utu (binadamu)

**2.2.4 Sifabia za Fasihi ya Watoto**

Kuna sifa za jumla ambazo ni sharti ziibainike katika fasihi ya watoto. Tutaeleza sifa moja baada ya nyingine tukitoa mifano mwafaka kwa kila moja.

**(i) Maudhui Rahisi**

Kigezo muhimu kinachotumiwa kubainisha fasihi ya watoto ni urahisi wa maudhui. Sharti fasihi ya watoto ieleweke ili mtoto aweze kupokea ujumbe wa mwandishi. Inadaiwa kuwa fasihi

yenye mawazo mazito kwa mfano ukoloni mamboleo, haihusu watoto kwani hawaelewi mambo ya ukoloni.

Maudhui katika fasihi simulizi na andishi sharti iendeleze kila kinachofahamika kwa mtoto. Irejelee mazingira yake kwa njia dhahiri- mazingira yenye milima, wanyama na ndege.

**ii) Kufurahisha**

Jukumu mojawapo la fasihi ni kuburudisha, kuliwaza na kufunza jamii. Hivyo, kwa namna ambavyo watoto hupenda michezo na mambo ya kuwafurahisha, kazi ya fasihi iwape furaha ndiposa wawe na hamu ya kuisoma na kupokea ujumbe wake. Kazi hizo zijumuishe nyimbo, mashairi ya kulumbana, michoro kwenye jalada na kurasa tofauti na rangi mbalimbali za kuvutia macho. Aidha, wahusika katika kazi hizo washiriki katika matendo mbalimbali. Kazi kama hizo ni kama hadithi ya King'ei *Tomorrow this time.*

**(iii) Wahusika**

Hawa ni binadamu, wanyama, mizimwi, inayohusika katika masimulizi au hadithi za maandishi kama vile ngano, vibonzo, vitendawili, methali, mafumbo, visakale, khurafa ili kuendeleza maudhui ya mwandishi.

Fasihi ya watoto itumie wahusika ambao ni vielelezo bora wa kuigwa. Iwapo wahusika waovu wamesawiriwa, ni vyema tabia zao ziweze kuadhibiwa ili wema uweze kushinda uovu.

Wahusika waweze kuwa na nguvu zinazowafanya watoto kujitambulisha nao. Aghalabu, watoto wanapotumiwa katika hadithi, huwafanya watoto kujijua zaidi ingawa hata wanyama, watu wazima na mijitu inaweza kupitisha ujumbe kwa watoto.

**(iv) Mazingira**

Fasihi ya watoto iweze kumulika mazingira rahisi yanayomzunguka mtoto ili aweze kuelewa fika. Iwapo fasihi imeandikiwa watoto wa mjini, haina budi kusawiri mambo wanayoyaelewa kama vile majumba ya ghorofa, watoto wa mtaani (chokora), magari na eropleni.

Iwapo mambo hayo yataandikiwa mtoto anayekulia vijijini, huenda akatatizika na kutofahamu. Hivyo sharti fasih ya watoto iakisi mazingira ili iweze kumkuza motto kwa kuelewa amali za jamii yake.

Mazingira ya mifugo, mazao, ushirkiano, bidii yanaweza kumulikwa katika ngano, mashairi ya maigizo na nyimbo.

**(V) Ubunifu**

Kazi ya fasihi inahusu ubunifu. Hata hivyo, Kingstone (1974) analaumu waandishi wanaotumia 'uhalisia-ndoto' katika kazi za

watoto. Anadai kwamba bunilizi huwatia watoto uoga na kuwaepusha na uhalisia, hali inayoathiri fikra zao kwa kuona ulimwengu kama usio wa kweli yaani wa kutisha!

Kingstone anapendekeza kuwa watoto wana uwezo wa kufahamu na kukubali hadithi za kihalisia zinazohusu maisha na mazingira yao. Hivyo, watoto wanahitaji kutagusana na motifu mbalimbali ambazo zinadhihirisha ukweli hata pale bunilizi hutumiwa.

Kwa namna watoto hupenda mambo ya kimazingaombwe, waandishi wa fasihi ni sharti wachanganye uhalisia na bunilizi kiasi ili kufanikisha utunzi. Hata katika jamii tofauti za Afrika, watoto walipata kupewa amali za jamii kupitia hadithi za "mijitu" ambazo zilijikita katika misingi ya bunilizi.

**(Vi) Mtindo wa Lugha**

Lugha ndio msingi wa fasihi. Ni chombo cha kupitisha ujumbe na bila lugha hakuna fasihi. Hivyo, ili itimize jukumu lake katika fasihi ya watoto ni sharti ieleweke kwa kuchuja msamiati unaosadifu umri, sentensi fupi (sahihi) ili lugha iafiki tajriba za watoto.

Msamiati mgumu, sentensi ndefu zenye vishazi, misemo, mafumbo mazito yaepukwe ili ujumbe ( na hamu ya kusoma) usitatizwe. Tashbihi, methali na mbinu ya mazungumzo zitumiwe lakini katika kiwango kidogo.

### (Vii) Umbo la Kitabu

Kitabu chochote kile cha watoto sharti kiwe na umbo la kuvutia lisilotamausha. Uzito wa kitabu ulingane na umri wa mtoto ili aweze kubeba bila ugumu wowote.

Hati za maandishi ziwe kubwa ili zisomeke bila shida. Aidha, karatasi ziwe za hali ya juu ambazo hazipasuki kwa urahisi. Jalada livutie kwa rangi tofauti tofauti za kupendeza pamoja na picha nzuri.

### (Viii) Ploti

Masimulizi ya hadithi yawe ya moja kwa moja ili mtoto asikanganyike. Pale ambapo kuna matukio tofauti, mwandishi atumie taharuki ili kumfanya mtoto kuwa na uchu wa kufuatilia hadithi. Mtindo wa taharuki ni maarufu sana katika sinema za watoto. Aidha, matumizi ya nyimbo ni muhimu ili kuondoa uchovu kwa msemaji hivyo matumizi yakatizwe na nyimbo ili kuibua hisia mpya.

Sifa hizo zote zilizojadiliwa hufanya fasihi ya watoto kuvutia na hivyo kufanikisha usomaji na upokezi wa maudhui miongomi mwa watoto. Hata hivyo, sifa ya lugha na maudhui ndio muhimu zaidi katika kubainisha fasihi ya watoto.

### 2.2.5 Uteuzi wa Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ikiwa ni pamoja na hadithi, methali, vitendawili, nyimbo, mazungumzo, ushairi, maigizo katika fasihi andishi au simulizi sharti yaakisi vipengele vifuatavyo:

**(i) Maudhui**

Maudhui yalingane na umri na mazingira ya watoto. Iwapo kazi inalenga jamii pana kama vile taifa, mambo ya kabila yaepukwe kwa kuchanganya majina ya makabila tofauti kama vile Onyango, Kariuki, Muruga na Kitheka ili kuumba upya maudhui na mazingira.

**(ii) Wahusika**

Wahusika katika fasihi wawe watoto au chochote kile ambacho mtoto anaweza kujitambulisha nacho ili kujielewa na kupata ujumbe kwa njia rahisi. Watoto wanaweza kutumika, mijitu, wanyama katika utambaji wa hadithi, maigizo mafupi na vitendawili.

**(iii) Ploti**

Huu ni mriririko wa vitushi. Aghalabu mtindo wa masimulizi ya moja kwa moja ni maarufu ili kuepuka utata. Mtunzi ajiepushe na mbinu nyingi kama vile kusengeranyuma, hadithi ndani ya hadithi, kwani huweza kumtatiza msomaji (mtoto).

**(iv) Lugha**

Uchaguzi wa lugha katika fasihi hutegemea umri wa mtoto. Mtindo wa sentensi sahili ndio maarufu. Pia matumizi ya uakifishaji mchache, hati kubwa na maelezo.

**V) Umri wa Mtoto**

Uteuzi wa kitabu, kipindi cha redio au runinga, sinema hutegemea umri wa mtoto. Hivyo, kiwango cha lugha na maudhui katika sanaa vilingane na umri wa mtoto ili asifunzwe mambo tata. Yanayoandikwa kwa ajili ya mtoto yatokane na mazingira yake halisi.

**Vi) Umbo la Kitabu**

Namna kazi ya fasihi imechapishwa, saizi, picha za jalada na rangi ni muhimu. Hati zisomeke, michoro iwepo katika kurasa mbali mbali ili irahisishe uelewaji wa ujumbe katika kazi hiyo.

**Hitimisho**

Katika kutamatisha sifabia za fasihi ya watoto, ni muhimu kutambua kwamba zinalingana na kiwango cha umri. Watoto wa shule za chekechea wanafaa kwa sifabia ambazo zimepitiwa katika kazi hii. Ikiwa umri utabadilika, sifabia hizi zinaweza kubadilika pia.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kwa hivyo yule anayetafiti kazi za watoto inambidi aonyeshe kiwango cha umri anaotafitia ili msomaji wake asitatanike anaposoma kazi yake.

# SURA YA TATU

## MTINDO WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA NYIMBO ZA WATOTO WA SHULE ZA CHEKECHEA

### 3.0 Utangulizi

Sura hii ndio upeo wa juu wa kazi hii ambayo inachanganua data ya utafiti.

Lengo kuu la sura hii ni kuchanganua mtindo uliotumiwa katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea kupitisha ujumbe kwa walengwa wao. Walengwa wenyewe ni watoto wanaoziimba nyimbo hizi. Ili kutimiza lengo hili, vipengele vifuatavyo vimeshughulikiwa:-

(i) Kipengele cha maudhui
(ii) Kipengele cha sentensi
(iii) Kipengele cha msamiati
(iv) Kipengele cha tamathali za usemi.

Tutajadili aina za maudhui yaliyoshughulikiwa katika nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea. Kupitia kwa maudhui haya, tutaweza kupata mbinu zilizotumiwa katika kuyawasilisha. Mbinu hizi ni sentensi, msamiati na tamathali za usemi. Ili kuwasilisha maudhui, msanii huchagua aina ya sentensi atakazotumia, msamiati na hata tamathali za usemi. Katika kuangalia mbinu hizi, maelezo haya yanatupatia mwangaza wa kile tunatafiti kuhusu mbinu hizi.

### 3.1.0 Maudhui katika Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea

Maudhui yaliyowasilishwa katika nyimbo hizi za shule za chekechea hutegemea silabasi yao. Mwalimu huchagua wimbo kulingana na somo ambalo atasomesha. Kutokana na maelezo ya walimu hawa katika utafiti wetu, walidokeza kuwa nyimbo hizi zimetungwa kupitia kwa utaratibu huu wa masomo yao. Hata hivyo kuna nyimbo zingine ambazo zinaimbwa kwa ajili ya kufurahisha watoto bila kuwa na lengo lolote la kuwaelimisha. Haja yetu ya ufafiti itakuwa kwa zile nyimbo ambazo maudhui yake yametambulikana; zile ambazo ni za kufurahisha hatutazitafitia.

### 3.1.1 Maudhui ya Elimu

Maudhui ya kielimu yalishughulikiwa katika nyanja tofauti tofauti. Katika wimbo wa *Twapenda mambo yote* twaona jinsi maudhui hayo yamewasilishwa ambapo muwasilishi anaelezea jinsi watoto wanavyopenda mambo yote yanayotendeka shuleni. Mifano ya mambo hayo yamewasilishwa kama vile kujua kusoma ambapo anasema *waona furaha.* Mfano mwingine ni ule wa *kuimba vyema.*

Pia katika wimbo wa *a,e,i,o,u* wanafunzi wanadhamiriwa kusoma herufi hizi ambazo twafahamu ndio msingi wa elimu ya watoto wa shule za chekechea. Hapa wimbo wawasilishwa kwanza kwa kuelezea mtoto anavyotakiwa kujua kuzitamka herufi hizi. Baada ya kuzitamka herufi kwa herufi anatakikana kuzitamka kupitia maneno ambayo yametumika katika wimbo huu. Maneno yenyewe

ni angalia inayowasilisha herufi *a*, enda inayowasilisha *e*, ingia inayowasilisha *i*, ondoka inayowasilisha *o*, na mwisho usiende inayowasilisha *u*.

Baada ya watoto hawa kujua herufi katika lugha ya Kiswahili, pia wimbo wa *imwe munyanyae wa ili* umeendeleza nambari. Hapa mtoto anafunzwa nambari za kuhesabu ambazo pia ni msingi wa elimu ya watoto. Nambari hizi ni *1,2,3,4,5,6,7,8,9,10*. Msanii anatumia mtindo wa uhusiano wa herufi hizi ambapo twaona moja ikiwa rafiki wa pili, pili ikiwa rafiki wa tatu, tatu ikiwa rafiki wa nne, nne ikiwa rafiki wa tano, tano ikiwa rafiki wa sita, sita ikiwa rafiki wa saba, saba ikiwa rafiki wa nane, nane ikiwa rafiki wa tisa,na tisa ikiwa rafiki wa kumi.

Pia katika maudhui haya ya elimu wimbo wa *Syana sya nasali* unaashiria kuwafunza watoto hali ya kutafsiri ambapo maneno kama vile *mwalimu* yametafsiriwa kuwa *teacher* katika lugha ya Kiingereza, *kivila* (kiti) kama *chair*, *ndilisya* (dirisha) kama *window* na kwoko (mkono) kama *hand*.

### 3.1.2 **Maudhui ya Umuhimu wa Mama kwa Mtoto**

Maudhui ya umuhimu wa mama kwa mtoto yameendelezwa katika baadhi ya nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Nyimbo nyingi zawasilisha mama kama mtu ambaye ana umuhimu mwingi kwa mtoto hasa katika upande wa chakula.

Katika wimbo wa *Mama yangu ameniacha* unadhihirisha umuhimu huu kwamba mama akiwa hayupo nyumbani mtoto hawezi akalala; kwamba mama ndiye humpikia chakula na akiwa hayupo mtoto atashinda njaa. Pia hali hii yadhihirika katika wimbo wa *Mama nipe mayai*. Hapa twaona mama ndiye anayejua lishe bora. Mtoto anawakilishwa akiuliza mayai badala ya uji. Mtoto anasema kwamba amechoka kwa kunywa uji pia amechoka kwa kula ugali na kabeji. Sasa anataka lisho bora ambalo ni nyama, mboga, mahindi, maziwa na matunda ambalo akitumia atakuwa mbali na magonjwa. Anayehitajika kutafuta chakula hiki ni mama bali si mwingine kulingana na wimbo. Kupitia kwa wimbo huu pia, mtoto atakua akijua chakula kinachofaa maishani ni kipi.

### 3.1.3 Maudhui mengineyo

Maudhui mengine tofauti yamewasilishwa kupitia kwa nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea. Wimbo wa *Taifa lenye nguvu* umewasilisha maudhui ya taifa letu ambapo vyama vya nchi yetu vyawasilishwa kukiwa na nia ya watu wote waungane. Mtu akiwa katika chama cha K.A.NU, FORD au D.P ahitajika kuungana na wale wengine ili wajenge nchi yenye nguvu. Watoto watakuwa wakijua watu wanahitajika kuungana ili wajenge nchi nzuri.

Katika wimbo wa *Andu ala matasomaa* umewasilisha maudhui ya ushauri kwa watoto kwamba akikosa kusoma atataabika sana. Watoto hawa hushinda wakitangatanga wakifafuta chakula, usiku ukifika wanaiba mahindi ya wenyewe. Wimbo wa washauri watu

kama hao si wa kuheshimu. Mtoto hatapenda kutosoma kwa sababu akikosa kusoma atakuwa mfano unaodokezwa na wimbo huu. Tena wimbo wa *Soma soma hee* wawasilisha mfano wa maudhui haya ya ushauri kwamba mtoto anatakikana kufanya kile kinachohitajika kwa wakati unaofaa. Kama ni wakati wa kusoma asome , kama ni wakati wa kuimba, aimbe, wakati wa kucheza , acheze, na wakati wa kuchora achore.

Mwisho kuna wimbo wa *Nyumba ni nzeo*, ambao wawasilisha maudhui ya kile kinachotumiwa kujenga nyumba nzuri. Katika nyumba hii nzuri huwa na dirisha, mlango, kuta , paa, pamoja na miti iliyopandwa nje ya nyumba hiyo. Nyumba hii nzuri ndimo kila mtu huishi. Hapa mwandishi anataka mtoto kufahamu mazingira ya nyumba ili aelewe nyumba anayokaa.

## 3.2 Maelezo ya Sentensi kwa Jumla

### 3.2.0 Kiwango cha sintaksia

Crystal na Davy (1969) ndio waliopendekeza kiwango hiki cha sintaksia.

Tuki (2004: 46) wanasema kuwa;

> Sintaksia ni tawi la isimu linalojihusisha na mahusiano baina ya maneno katika tungo.

Kulingana na maelezo ya Tuki (2004) na hata Crystal na Davy (1969) kiungo kilicho muhimu sana ni sentensi ambapo twafaa tuangalie uhusiano uliopo baina ya maneno katika tungo. Kiwango hiki kwa hivyo ni muhimu sana katika uchanganuzi wa fasihi.

Sentensi hapa itategemea ni ya aina gani; cha muhimu ni kwamba sentensi itaitwa sentensi kama itaeleza fikira au hisia kwa kutumia neno moja au zaidi. Kanuni za kisarufi za lugha maalum ndizo hutawala sentensi.

Katika matumizi ya sentensi, msanii anaweza kutumia aina tofauti tofauti za sentensi kulingana na jambo au dhana anayotaka kuelezea. Kwa hivyo, tutaangalia aina za sentensi ambazo msanii anaweza kutumia.

### 3.2.1 Matumizi ya Sentensi Fupi Fupi

Sentensi huundwa na msanii kwa uangalifu ili aweze kuwasilisha hoja yake kwa njia mwafaka inayoweza kueleweka na msomaji au msikilizaji wake.

Sentensi fupi fupi huwa ya neno moja, mawili au matatu na huweza kubeba hoja moja.

Mohammed (1995) anasema kwamba;

> Sentensi fupi fupi hutumika kujenga taathira ya utendaji, na kwamba sentensi hizi fupi fupi huweka makato ya mikazo na mitegezo, mipando na mishuko ya sauti yenye vipimo vya masafa mafupi na hili husababisha sehemu hiyo kusikika au kusomeka kwa mtitimo wa haraka haraka ambao unakwenda kwa hisia inayotengwa.

Kulingana na maelezo haya, mtitimo huo huwezesha kusaidia kubainisha uchangamfu, harakati, woga, hofu, wasi wasi. Hizi ni hali ambazo tunakumbana nazo katika uimbaji.

### 3.2.2 Matumizi ya Sentensi Ndefu Ndefu

Sentensi ndefu ni ile ambayo itabeba hoja zaidi ya moja. Pia huweza kuwa na maneno zaidi ya matatu. Kuna aina mbili za sentensi ndefu, yaani zile changamano na ambatani.

Mohammed (1995) anasema kwamba;

> Sentensi ndefu ndefu zinapunguza mwendo wa mtitimo na hivyo kumfanya msomaji adodee anaposoma kwa utaratibu.

Wambua (2001) anasema kwamba;

> Sentensi ndefu ndefu hutumiwa kuwasilisha ujumbe wenye huzuni, uvivu, ama wenye kukinai.

### 3.2.3 Matumizi ya Sentensi zenye Miundo Huru

Sentensi zenye muundo huru ni zile ambazo hazifuati kanuni za utunzi wa sentensi. Kwa msanii, sentensi hizi hubeba maana maalum ambayo ingefaa kuwasilishwa kupitia kwa sentensi ya aina hii. Mara nyingi matumizi ya sentensi za aina hii hupatikana katika mashairi. Kwa vile nyimbo ni mfano wa ushairi, basi sentensi za aina hii hutumika na utapata msanii ataweza kupitisha ujumbe wake kwa njia mwafaka na analoweza kueleweka kwa urahisi.

## 3.3.0 Aina za Sentensi katika Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea.

### 3.3.1 Sentensi Ndefu Ndefu

Sentensi inakuwa ndefu katika wimbo pale maneno zaidi ya manne yanatokea katika sentensi moja. Sentensi za aina hii zimetokea katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea . Sentensi hizi zinatumiwa kwa madhumuni maalaum bali si tu hivi hivi. Mahali ambapo madhumuni yameeelwzwa kihadithi, sentensi ndefu hutumika. Matumizi ya sentensi hizi pia yanatokea wakati mwandishi anapojaribu kuelezea jambo Fulani.

Wimbo wa Twapenda mambo yote unadokezea jinsi watoto wanavyopenda mambo yote ya shule. Nia au lengo la wimbo huu ni kutahadharisha watoto kuona furaha wanaposoma.

Wimbo unasema,

*Twapenda mambo yote ya shule kabisa,*

*Kujua kusoma twaona furaha.*

Wimbo wa *Twapenda mambo* yote unadokezea jinsi watoto wanavyopenda mambo yote ya shule. Nia au lengo la wimbo huu ni kutahadharisha watoto kuona furaha wanaposoma.

Wimbo unasema,

*Twapenda mambo yote ya shule kabisa,*
*Kujua kusoma twaona furaha.*

Mwandishi ametumia mtindo wa kuelezea ili kudokezea maudhui yake ambayo ni kuhimiza watoto kupenda kusoma. Matumizi ya sentensi ndefu ndefu yanapatikana katika wimbo huu. Lengo kuu ni kuelezea jinsi taifa lenye nguvu linahitajika kwamba ni lile ambalo watu wake wamenganika. Hata watu wakiwa katika vyama mbalimbali kama vile chama cha KANU, cha FORD na DP wanahitajika kuungana kama taifa moja. Maudhui haya yanapitishwa kwa kutumia sentensi ndefu ndefu,

Mfano;

*Taifa lenye nguvu ni taifa ambalo watu wameungana*
*Uu uu tuungane tujenge taifa lenye nguvu*
*Watoto wa Kenya, sisi tunataka taifa moja.*

Katika vifungu hivi viwili, twaona maudhui ya muungano wa watu wa Kenya yakipitishwa kwa sentensi ndefu. Watoto wanalengwa kuwa wanataka nchi au taifa moja lisilo na mgawanyiko. Mtoto huyu atakua akielewa kuwa kila mwananchi ni kitu kimoja.

Matumizi ya sentensi ndefu ndefu yanadhihirika pia katika wimbo wa andu ala matasomaa. Hapa twaona matumizi ya hadithi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

yakitumiwa sambasamba na maelezo ya mwimbaji. Wimbo unahadithia jinsi watu wasiosoma wanataabika sana. Mwandishi anaelezea taabu mtu huyu anazokumbana nazo kama vile kutangatanga wakitafuta chakula, usiku ukifika wanaiba mahindi ya watu na kwamba watu kama hao hawana heshima.

Wimbo unaendelezwa hivi;

*Wale hawasomi hutaabika sana,*
*Hushinda wakitangatanga wakitafuta chakula,*
*usiku ukifika wanaiba mahindi ya watu,*
*watu kama hao hawana heshima.*

Pia katika wimbo wa *Nyumba ni nzeo* matumizi ya sentensi ndefu ndefu yamedhihirka. Hapa Matumizi ya hadithi yanachanganywa na maelezo,

*Nyumba ni nzuri*
*Nyumba ya kuishi*
*Mlango, dirisha pamoja na paa, kuta*
*na miti iliyopandwa nje*
*nyumba ni nzuri*
*Nyumba ya kuishi*
*Ndipo kila mtu hujificha.*

### 3.3.2 Sentensi Fupi Fupi

Matumizi ya sentensi fupi katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea yameteuliwa kwa umaarufu sana. Sentensi hizi zimetumika kwa makusidi maalum katika kuwasilisha ujumbe

uliokusudiwa. Sentensi za aina hii hutumika mara nyingi katika kipokeo cha wimbo. Kipokea au kiitikio hiki huwa kinasisitiza ujumbe wa wimbo.

Mfano wa wimbo ulio na kipokeo cha aina hii ni ule wimbo wa *Mama yangu* ameniacha.

Wimbo huu una vipokeo tofauti tofauti ambavyo vimetumiwa kama maelezo ya jinsi mtoto anafurahia wakati mama yake anapompikia chakula mpaka wakati unapofika wa kupewa chakula ale na mama. Katika vipokeo hivi, wimbo unasema;

*Tiririri mama X2*
*Oh tiririri mama X 2*
*Pika chakula mamax2*
*Pika chakula mamax2*
*Oh pika chakula mama x2*
*Songa na mwiko mamax2*
*Nipe nikule mamax2*
*Oh nipe nikule mamax2*

Wakati mtoto anaimba *tiririri mama* huwa anacheza cheza huku akionyesha furaha kwa ajili ya kupikiwa chakula na mama. Hali hii inaathiri mtoto pamoja na kufanya hadhira yake kupata nafasi. Sentensi fupi fupi ndizo zinaweza kuwasilisha hali ya aina hii.

Matumizi ya sentensi fupi pia yametumika katika wimbo wa *Maji ni maisha* katika wimbo huu nayo imerudiwa katika maneno tofauti tofauti ili kusisitiza jinsi maji yalivyo na umuhimu maishani mwa binadamu. tazama hali hii vile inavyotokea;

*Tunapika nayo*
*Tunaoga nayo*

Kukariri kwa neno hilo *nayo* kumemfanya mtoto kuelewa kwa undani umuhimu wa maji jambo ambalo halingefanyika kama sentensi fupi haingetumiwa. Matumizi ya aina hii ya sentensi fupi yanatokea katika wimbo wa *Yesu ni kana kaseo*. Hapa neno alisaidia limetumika mara kadhaa katika maneno tofauti tofauti. Hivi ndivyo inavyotolea:-

*Alisaidia mama yake*
*Alisaidia mama kazi*
*Alisaidia baba Yusufu*

Neno hili *alisaidia* inasisitiza vile aliweza kusaidia wazazi wake jambo ambalo linachangia kuelewa kwa mtoto umuhimu wa kusaidia wazazi wake. Pia sentensi fupi zatokea katika wimbo huu wakati wa maelezo ya aina za kazi alizoweza kusaidia wazazi wake. Yesu aliweza kusaidia mama yake kuosha vyombo na pia baba yake Yusufu katika kupiga randa kama vile wimbo unavyoeleza:-

*Alisaidia mama yake kuosha vyombo,*
*Alisaidia baba Yusufu kupiga randa,*

Ni dhahiri na shahiri kuwa shabaha kuu ya kutumia sentensi fupi katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea ni kutaka ujumbe uzame katika akili za watoto hawa kwa urahisi kinyume kama sentensi ndefu zingetumika ambazo hutoa maelezo mengi.

### 3.3.3 Sentensi Tongole

Sentensi tongole ni zile ambazo zimetongolewa katikati au mwishoni badala ya kuumbwa kwa muundo uliomo katika wimbo husika. Mbinu hii ya sentensi tongole haikutumika sana katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea, isipokuwa tu katika wimbo mmoja imejitokeza wazi wazi. Mbinu hii imeweza kutumiwa vizuri kwa sababu siyo kila mwimbaji anaimba bali ni sauti ya wavulana ambao sauti yao ina toni nzito ukilinganisha na ya wasichana. Lengo la kutumia sauti hiyo ya wavulana ni kubadilisha mdundo na pia hali ya kuepusha matumizi ya sauti moja tu kuanzia mwanzo hadi mwisho kama vile mwalimu Theresia Musyoka kutoka shule ya chekechea ya Ngomeni alivyoelezea;

> Matumizi ya sentensi tongole huweza kubadilisha
> sauti katika wimbo na hali hii husaidia ujumbe ueleweke zaidi.(1)

Pia mwishoni mwa wimbo, ungesikia watoto wakicheka pamoja na wasikilizaji kuonyesha kuna hali tofauti ya kupendeza imetokea. Mfano wa kauli hii kama vile tumeelezea imetokea katika wimbo mmoja uitwao *Andu ala matasomaa* ambapo neno *Andu* (watu) ndilo limetongolewa mwishoni mwa wimbo.

*Andu ala matasomaa mathinaa muno,*
*Maitinda maitangatanga maimantha kya kuya,*
*Utuku wavika maitula mbemba syeene,*
*Andu tasu ti mandaia*
*Andu!*

*"Watu wale hawasomi hutaabika sana*
*Hushinda wakitangatanga wakitafuta chakula*
*Usiku ukifika wanaiba mahindi ya wenyewe*
*Watu kama hao si wa kueshimiwa*
*Watu!.*

Neno ambalo limetongolewa *watu* huwa linasemwa bali haliimbwi. Nia ni kutoa msisitizo wa watu hawa ambao hawasomi kwamba si watu wazuri. Kupitia kwa msisitizo huo, mtoto ataweza kuelewa kuwa si vizuri kutosoma asiwe kama mfano wa watu hawa.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 3.4 Sentensi Zilozobadilika muundo wa mpangilio wa Maneno

Sentensi hizi ni zile zilizobadilika mpangilio wa maneno katika nafasi mbali mbali za mlalo wa sentensi ambapo maana yaweza kubadilika au msisitizo fulani kutokea. Mahali mabadilisho haya ya muundo wa sentensi yametokea katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea, msisitizo fulani hutokea hapo. Katika wimbo wa *Twapenda mambo yote*, twapata mfano mzuri wa sentensi ya aina hii. Sentensi inasema *kujua kusoma twaona furaha* Msisitizo katika sentensi hii ni kujua kusoma, ambapo unasema, kuwa *twaona furaha.* kama sentensi hii ingekuwa twafurahia kujua kusoma msisitizo ungekuwa tofauti.

Katika wimbo wa *Mama nipe mayai* kauli ya aina hii imetumika wimbo unaposema;

*Kazi zetu twafanya, na kucheza twacheza*

Sentensi hii inasisitiza hali mbili tofauti ambapo msisitizo wa kwanza ni kazi na wa pili ni kucheza. Kama sentensi hii ingetanguliza kwa kutumia kitenzi " kufanya" na kuondoa kitenzi cha mwisho cha "kucheza" basi sentensi hii ingetafrisrika tofauta na vile ilivyo sasa.

Msisitizo pia wapatikana katika wimbo wa *soma soma soma* ambao una sentensi zilizo na muundo uliobadilika, wimbo unasema

*Soma soma soma wee x2*

*Wati wa kusoma soma wee x2*

*Imba imba imba wee*

*Wakati wa kuimba imba wee*

*Cheza cheza cheza wee*

*Wakati wa kucheza cheza we*

*chora chora chora wee*

*Wakati wa kuchora chora wee.*

Maneno *soma, cheza, imba* na *chora* yamebandikwa hili kuleta msisitizo wa kile mwandishi anasema. Kama sentensi hizi zingebadilishwa na kuwa;

*Wakati wa kusoma wahitajika kusoma*

*Wakati wa kuimba wahitajika kuimba*

*Wakati wa kucheza wahitajika kucheza*

*Wakati wa kuchora wahitajika kuchora*

Msisitizo hapa ungekuwa tofauti na vile ulivyo hapa juu. Katika mabadiliko hayo, msisitizo ni mwepesi kuliko ulivyo katika wimbo. Kauli hii inamwezesha mtoto kufurahia zaidi kile kinachowasirishwa na wimbo.

### 3.4.0 Jinsi Msamiati Ulivyoteuliwa

#### 3.4.1 Utangulizi

Kabla ya kuangalia msamiati uliotumika katika nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea, kwanza tumeangalia kwa jumla ni

aina gani ya msamiati tunahitaji kuangalia. Pia tumeelezea maana ya kila aina ya msamiati ulioelezwa na ambao tunakusudia kukumbana nao katika nyimbo hizi.

### 3.4.2 Msamiati kwa jumla

Dhana hii ya msamiati ni muhimu sana katika uchanganuzi wa matini yoyote. Tuki (2004-272) wanaeleza msamiati kama jumla ya maneno katika lugha fulani kwa hivyo maneno yote yaliyoko katika lugha yoyote ama matini yoyote ndiyo yanaitwa msamiati; lakini kuna msamiati teule na ule ambao sio teule. Msanii anatumia msamiati wa aina tofauti kupitisha ujumbe wake. Msamiati teule ni ule mgumu ambao msanii ameuteua kwa nia fulani na hapa ndipo anapopimwa kupitia jinsi anavyowasilisha hoja zake. Msamiati usioteule ni ule wa kawaida unaopatikana katika lugha au matini yoyote.

Mohammed (1995) akijadili dhana hii ya msamiati anadokeza kuwa ubora wa maneno na uteuzi wake pamoja na mpangilio wake umo katika kupata maana na taathira za kisanaa za maneno yanayotumiwa. Hapa anajaribu kupitisha hoja kuwa neno moja halitakuwa na muhimu bali thamani yake hupatikana katika matumizi yake pamoja na muktadha. Kwa hivyo jinsi maneno yanavyopangwa katika kazi yoyote ya sanaa ni muhimu sana kwa sababu uteuzi au mpangilio huu wa maneno katika sentensi huweza kubadilisha maana, kuzua utata fulanai, kuweza hata kuleta hali ya kutoeleweka kile kinachozungumziwa.

Tunapozingatia kazi ya utunzi utatambua kwamba kuna aina nyingi za maneno ambayo mtunzi anaweza kuteua katika kuendeleza kazi yake. Baadhi ya maneno hayo ni kama:

(a) Visawe:- haya ni maneno mawili au zaidi yanayokaribiana sana kimaana. Utumiaji wa visawe katika kazi yoyote ya msanii hudhihirisha jinsi msanii huyo alivyokomaa katika lugha kwamba ana uwezo wa kucheza na maneno tofauti tofauti bila shida yoyote. Hali hii huweza kuondoa shida ya uchovu kwa msomaji kwa kutorudiarudia maneno na hivyo kuvutia katika kuendelea kusoma kazi yake.

(b) Msamiati wa adabu:- kulingana na Tuki(2004) neno adabu lamaanisha tabia njema, nidhamu, heshima, staha. Kwa hivyo tunapozungumzia msamiati wa adabu twatambua kwamba ni maneno ambayo yalipendekezwa kutumiwa katika muktadha fulani kuleta heshima fulani, Mifano ya maneno kama hayo ni kama vile; tafadhali, pole, asante, shukrani na kadhalika.

(c) Msamiati wa lakabu; haya ni majina ambayo mtu hujipatia au hupewa mbali na jina lake hasa; aghalabu huwa majina ya kutania. Majina ya kupanga. _Pia majina haya yaweza yakawa ni mafungu ya maneno au neno moja lenye maana iliyofumbwa. Msanii anaweza kutumia majina ya aina hii akiwa na lengo la kupitisha ujumbe wake kwa hadhira yake

kama ameona utatolewa kupitia maneno au majina ya aina hii.

(d) Msamiati wa mkopo; haya ni maneno yaliyotolewa kutoka lugha nyingine hadi ile inayotumiwa kutunga kazi. Msanii anaweza kuyakopa jinsi yalivyo au kuyabadilisha kupitia lugha anayotumia katika kazi yake. Mifano ya maneno kama haya ni kama:

| *Kiingereza* | *Kiswahili* |
|---|---|
| Television | Televisheni |
| Radio | Redio |
| Computer | Kompyuta |
| Cupboard | Kabati |
| Syllabus | Silabasi. |

Kupitia kwa aina ya misamiati ambayo tumeona, msanii atakuwa na uwezo wa kuchangua maneno anayotaka katika kuwasilisha ujumbe wake; yawe ni maneno ya lakabu, visawe, kukopa, au ya adabu na mengine mengi. Hali hii inadhihirika katika uchnganuzi wa watunzi hawa.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 3.4.3.0 Uteuzi wa Msamiati katika Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea

#### 3.4.3.1 Kuchanganya Ndimi

Matumizi ya kuchanganya ndimi yanatokea wakati maneno au sentensi zenye muundo uliovunja kanuni za kijamii za lugha husika zimetumika katika kifungu fulani. Hali hii hutokea wakati maneno ya lugha nyingine huingizwa katika kazi inayoshughulikia lugha tofauti na hiyo. Mfano nzuri ni maneno ya kiingereza kutumika wakati kazi Fulani inajihusisha na lugha ya Kiswahili. Hali hii imetokea vizuri katika wimbo wa *syana sya nasali* ambapo wimbo unahusisha lugha ya kikamba na papo maneno ya kiingereza yanatokea. wimbo unasema;

*Syana sya nasali tusomei nesa*
*nitwisi kisungu yes yes no.*
*Teacher ni mwalimu*
*Chair ni Kivila*
*Window ni ndilisya hand ni kwoko.*

*"Watoto wa nasari tusomeni vizuri*
*Tunajua kusoma kiingereza, yes yes, no*
*Teacher ni mwalimu*
*Chair ni Kiti*
*Window ni dirisha*
*Hand ni mkono".*

kupitia kwa kuchanganya ndimi twaona mafunzo ya kutafsiri yakipitishwa kwa mtoto vizuri sana pale ambapo mtoto ataweza kuelewa mwalimu aitaji kwa kiingereza, kiti kwa kiingereza, dirisha kwa kiingereza, na mkono kwa kiingereza matumizi ya kuchanganya ndimi yametokea katika wimbo wa watoto wema njooni.

Wimbo wasema:-

*Watoto wema njooni tosome*
*Sikiliza kengele*
*Ding dong ding.*

Matumizi ya mlio wa kengele yametumika kama hali ya kuchanganya ndimi kwa sababu tunaona kanuni ya lugha ya Kiswahili ya kuandika haikutumika. Maneno ding dong ding yametumia mtindo wa kiingereza.

Wimbo wa *Taifa lenye nguvu* umetumia mtindo wa kuchanganya ndimi. Hali hii imetokea katika kuandika maneno kwa ufupi yaani kiakronomia. Wimbo unasema:-

*Taifa lenye nguvu ni taifa ambalo*
*watu wake wameungana*
*Uwe mwana KANU*
*Uu mwana KANU*
*Uwe mwana FORD*

*Uu mwana FORD*

*Uwe mwana DP*

*Uu mwana DP*

Maneno yaliandikwa kwa ufupi kama vile KANU, FORD na DP yametumia mtindo wa kiingereza kama vile tulivyodokeza hapo juu.

**3.4.3.2 Msamiati wa Misimu**

Msamiati wa misimu hupotea baada ya kipindi fulani ingawa mchache hubaki na kutumiwa na jamii kwa kipindi fulani. Msamiati wa aina hii waweza kuwa maneno au semi na haja yake hasa huwa ni kurutubisha lugha msemaji au mwimbaji aweze kueleweka zaidi.

Katika wimbo wa *mundu utesi kuthamba* neno *kithingo* limetumika. Mwandishi anatumia neno hili kumaanisha wingi wa kile kinazungumziwa. Wimbo unasema katika kifungu hiki kwamba:

*Mundu utesi kuthamba ni ndia yi kithingo*

*Mtu asiyejua kuoga ana wingi wa ujinga.*

Kifungu hiki kinamaanisha kwamba mtu asiyejua kusoma ni mjinga kabisa kwamba hana mbele wala nyuma. Neno hili ndilo lililofaa kutumika katika kifungu hiki kwa sababu kama

angetumia neno lingine, ujumbe haungetokea vizuri na kueleweka zaidi. Neno hili halitumiki na limepotea katika msamiati wa kikamba.

Pia katika wimbo huu wa *Mundu utesi kuthamba*, maneno haya ya msamiati wa misimu yametokea katika sentensi inayosema:- *ni kana nithwe ni mutheu kw'u, kw'u, kw'u* yanaleta maana ya usafi wa hali ya juu. Mwandishi anayatumia mtoto aweze kuelewa ama kupata yale anayosema ikiwa atazingatia yale yote anaelezea kuhusu mtu anavyohitajika kufanya ikiwa anataka kuwa msafi. Maneno haya yanapotea pole pole siku hizi na badala yake tunatumia maneno *vyu vyu vyu* kuleta maana sawa.

**Tanbihi**

(1) Mahojiano haya yalipatikana kutokana na mahojiano yetu na mwalimu Theresia Musyoka wa shule ya chekechea ya Ngomeni mnamo tarehee 19/10/2006.

# SURA YA NNE

# MATUMIZI YA TAMATHALI ZA USEMI KATIKA NYIMBO ZA WATOTO WA SHULE ZA CHEKECHEA

## 4.0 Utangulizi

Katika sehemu hii tutajikita katika aina mbalimbali za tamathali za usemi ambazo zimetumiwa katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea.

Kabla ya kuingilia swala hili, kwanza tumeangalia tamathali za usemi kwa jumla huku tukielezea maana yake kulingana na wasomi mbali mbali. Baada ya kufanya hivyo, tumechunguza baadhi ya tamathali ambazo zimetumika katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea.

## 4.1 Maelezo ya Tamathali za Usemi

Uchanganuzi wa fasihi pia wahitaji kuangalia jinsi msanii ameimudu lugha. Mtindo hudhihirika kupitia uwezo huo wa mtunzi wa kutumia lugha jambo ambalo humfanya kuwa tofauti na wasanii wengine. Matumizi ya tamathali za usemi mtunzi uwezo huu wa ubunifu.

Mulokozi (1989) anasema:

> Tamathali za usemi ni tungo au kauli fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo ya kijamii.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kulingana na Mulokozi (1989) tungo hizi hujaribu kuchora picha kwenye akili ya msomaji ili kumwenzesha kuelewa ujumbe kwa urahisi kwani hufuma hisia zake. Hali hii hutokea kwa sababu huweza kubeba maneno machache lakini yakaweza kutoa maana ya upana mkubwa.

1. **Methali**

Huu ni usemi mfupi ambao huwa na maana nzito ya busara ndani yake.

Tuki (2004:240) anasema yafuatayo kuhusu methali;

> Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.

Wambua (2001) anasema kuwa methali zimegawika katika majopo tofauti tofauti kama vile, zenye mawaidha, majuto, kashfa, kejeli, shutuma, kuonya. Huwa ni sentensi zenye sehemu mbili ambazo hutegemeana. Sehemu ya kwanza huwa ni ya kuonyesha kinachotakikana, nayo ya pili ni matokeo ya kufuata au kutofuata maagizo hayo.

Jambo lingine muhimu ni kwamba mtunzi wa methali huwa hajulikani kwa sababu ni za kijamii na kuwa huendelezwa na jamii iliyoitunga.

Mfano: - (i) Hasira ya mkizi, furaha ya mvuvi.

(ii) Mcheza kwao, hutunzwa.

2. **Kinaya**

Kulingana na Ruo Kimani Ruo (1989:74) kinaya ni tamathali ya usemi ambayo hukusudiwa. Unaweza kuwa unamsifu mtu fulani kuwa ni msafi wakati ni mchafu

Watu wa rika moja wanaweza kutumia kinaya wakiwa na mwelekeo wa kutoerevuka kile wanachotaka kusema

**3.Chuku**

Chuku ni mbinu ya kutilia chumvi ambapo sifa hulundikizwa ili kuonyesha uziada wa jambo. Wambua (2001) anasema kuwa chuku hutumiwa hasa wakati mtunzi anapoashiria mshangao au anapotaka kukuza jambo dogo kupita kiasi. Ameorodhesha aina tatu za matumizi ya chuku kama:

(i) Msemaji akisimulia tukio la kawaida kama vile jambo la kustaajabisha.

(ii) Jambo dogo hudunishwa kupita kiasi.

(iii) Jambo kubwa hukuzwa kupita kiasi.

4. **Takriri**

Ngure (2003) anaelezea takriri kama ule urudiaji wa silabi au sauti zinazolingana katika maneno yanayokaribiana kimatamshi.

Anasema kuwa wakati mwingine maneno yanaweza kubadilika. Kurudia neno, kifungu, vina au hata sentensi nzima katika matini ili kutia mkazo au msisitizo zaidi katika jambo aandikalo au asemalo ni jambo muhimu katika uimbaji.

Ruo Kimani Ruo (1989;85) naye ameelezea takriri kama urudiaji wa maneno ama silabi kwa madhumuni maalum.

**5. Misemo**

Tuki (2004:273) wanaelezea misemo kama fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalum ili kutoa maadili. Semi hizi huwa fupi na huweza kuelezea kwa muhtasari mawazo ambayo yangeelezewa kwa sentensi ndefu.

Mifano:-

i) aga dunia -kufa

ii) piga kalamu -simamisha mtu kazi

iii)ingia mafa -kuchukua mali au watoto wa ndugu aliyekufa.

**6. Misimu**

Kulingana na Ruo Kimani Ruo (1989:78) misimu ni aina za semi ambazo hutumiwa sana na watu mpaka zimefikia kiasi cha kuchujuka. Uzoefu wa matumizi ya misimu unaweza kuifanya ikubalike na jamii kama misemo ya jamii husika.

Mifano ya misimu ni kama:-

toa chai -kupatiana hongo

fuata nyayo-kuwa mwaminifu kwa serikali

**7. Tasfida**

Tasfida pia hujulikana kama tauria. Njogu na Chimera (1999) wamesema kuwa tasfida ni mbinu ambayo hutumia lugha safi ili maneno machafu yasitumike. Tasfida hutumiwa kwa nia ya kukwepa karaha na hivyo kumwezesha msanii kuandika au kusema dhana 'chafu' hadharani bila kuchukiza au kufanya moyo wa msikilizaji au msomaji uchafuke.

Unapotumia maneno hayo machafu, inadhihirisha kukosa adabu ya lugha; mifano ya Tasfida ni kama vile:-

| *Chafu* | *Safi* |
|---|---|
| Choo | haja |
| Kufa | kukata kamba |
| Kuzaa | Kujifungua |

**8. Tashbihi**

Tashbihi ni matumizi ya lugha ambapo kitu kimoja chalinganishwa na kingine kwa kutumia maneno ya ulinganishi kama vile "kama," "sawa na," "mithili ya" "ja" na "mfano wa".

Tuki (2004:398) wameelezea tashbihi kama usemi wa ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Vitu vinavyolinganishwa pamoja lazima viwe na ulinganifu wa sifa, umbo, tabia au sura. Sifa hizi ndizo zinaamishwa kutoka kitu kimoja hadi kingine. Mohamed (1995) anasema kuwa tashbihi

lazima iundwe kwa misingi inayokubalika kimantiki hasa kulingana na jamii.

Mfano: - 1. Ukweli ni kama msumeno hukata bila kususia nao ukweli hauna pingamizi yoyote.

2. Mjanja Kama sungura- mtu ambaye ni mjanja hawezi akaaminika.

**9. Majazi**

Majazi ni mbinu ya msanii ya kuwapa wahusika majina yanayooana na sifa au matendo yao. Tuki (2004:216) wameeleza majazi kama upaji wa majina kulingana na tabia ya mhusika. Kwa mfano, katika fasihi:

- Jina majivuno hupewa anayejidai.
- Jina fisi huashiria mlafi.
- Jina subira hupewa mtu anayesubiri.

**10. Mafumbo**

Kufumba ujumbe ni kuufutika au kuuficha ili atakaye kuupata achemshe bongo, afikirie kwa uzingatifu mwingi ili aupate.

Mtunzi hutimiza haja yake ya kuwasiliana bila kuwahusisha waliolengwa na ujumbe hasa wakati anapozungumzia mambo ambayo ni mwiko kuyataja hadharani.

Wambua (2001) akimnukuu Mulokozi (1989) anasema kuwa fumbo hubuniwa na msemaji kwa shabaha na hadhira maalum, na kwa hivyo ni tofauti na methali na vitendawili ambavyo ni semi za kimapokeo.

**11. Nidaa**

Mugambi (1992:134) anaelezea mbinu hii kama;

> Namna ya msemo wa mawasiliano au sauti ya
> mshangao aitumiayo msanii kudhihirisha maono
> yake ya ndani au kilio cha moyo.

Msemo huu waweza kutoa hisia za ndani za mhusika kwa kutoa sauti ya kilio ambayo yaweza kuwa ya mshangao, huzuni, furaha au chuki.

Mifano ya sauti hizi ni kama vile;

Inshala! -kukubali
Ya Rabi! - Kilio au masikitiko
Alhamdulilahi-Shukrani au furaha. Mtu anapopata zawadi, cheo, neema au huzuni ambapo anamaanisha sifa zote ni za mwenyezi Mungu.
La hasha! - Kukanusha jambo.

### 12. Balagha

Balagha ni mbinu ambayo hutumia maswali yasiyohitaji majibu au majibu yake yajulikana wazi. Tuki (2004) wameelezea balagha kama;

> Ustadi wa kutumia lugha ili kushawishi au kufurahisha. Nia au lengo la maswali hayo huwa si majibu ya maswali hayo bali ni kutilia mkazo ujumbe unaowasilishwa, kusisimua msomaji au msikilizaji, kuathiri moyo kwa kuchochea furaha, huzuni au chuki. Kupitia kwa maswali haya wahusika huweza kutanabahishwa na kuvutia uzingativu wao katika jambo muhimu analolenga mwandishi.

Mara nyingi mtindo huu hutumiwa katika mahubiri ama hotuba kwa lengo la kuchochea watu akili zao katika mwelekeo unaokusudiwa na mwandishi.

### 13. Jazanda

Jazanda ni matumizi ya lugha kimafumbo kwa kuipa dhana maana iliyo mbali na maana ya kawaida.

Mohammed (1990) anasema kuwa jazanda yaweza kujengwa kwa picha za masikizi za mguso, za maonjo au za mguso. Hapa anamaanisha kwamba ujenzi wa jazanda ni lazima uhusishe hisia za mwili. Ulinganishi wa jazanda huwa ni wa moja kwa moja.

Ngure (2003:163) anaeleza jazanda kama lugha inayochora picha ya mahali au vitu kwa kutumia tamathali za usemi. Mfano ni; " alikuwa na uso kama bahari kwa wimbi ya machozi". Tunachorewa uso wa mtu uliojaa machozi yanayotiririka kama mawimbi ya bahari.

## 4.1.0 Uteuzi wa Tamathali za Usemi katika Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea

### 4.1.1 Matumizi ya Takriri

Takriri hutokea hasa hasa kupitia marudio ya neno, sauti au maneno yale yale ili kutia mkazo zaidi juu ya jambo asemalo. Nia ya kutumia takriri ni kumfanya anayesikiliza au kusoma aelewe umuhimu ulio katika jambo linalokaririwa.

Matumizi ya takriri katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea yametokea kupitia hali tofauti tofauti ambazo tutaziangalia hapo chini.

#### (i) Matumizi ya Takriri Kifungu cha Maneno

Katika wimbo wa *Taifa lenye nguvu* fungu la maneno *uwe mwana* imetumiwa kusisitiza kujiunga katika chama fulani. Wimbo unasema:-

*Uwe mwana* KANU
uu KANU
*Uwe mwana* FORD

uu FORD

*Uwe mwana* DP

uu DP

Kwa kutaja vyama tofauti tofauti na kusema *Uwe mwana* ni kumaanisha kwamba vyama nchini ni vingi, lakini wahitajika kuungana na kuwa kitu kimoja.

Matumizi mengine ya takriri kifungu cha maneno yametokea katika wimbo wa *Soma soma soma* ambapo maneno *wakati wa* yamerudiwa mara kadhaa.

Wimbo unasema:-

*Soma soma soma wee*
*Wakati wa kusoma soma wee*
*Imba imba imba wee*
*Wakati wa kuimba imba wee*
*Cheza cheza cheza wee*
*Wakati wa kucheza cheza wee*
*Chora chora chora wee*
*Wakati wa kuchora chora wee.*

Wimbo hapa unaposema *wakati wa* mwandishi anasisitiza kipindi fulani cha kufanya jambo fulani. Lengo kuu ni kuhimiza msikilizaji kuzingatia kile anachofanya.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**(ii) Matumizi ya Takriri Neno**

Matumizi ya takriri neno yametokea katika wimbo wa *Mama yangu ameniacha* ambapo neno *Mama* limetumika karibu kila mstari ili kusisitiza hali tofauti zinazopitiwa na mama akipika chakula mpaka kumlisha mtoto. Anasisitiza kuwa mama anahijajika kupika chakula na baada ya hayo, kumlisha mtoto; wimbo unasema:-

*Tiririri mama x2*
*Oh tiririri mama x2*
*Pika chakula mamax2*
*Oh pika chakula x2*
*Songa na mwiko mama x2*
*Oh songa na mwiko x2*
*Nipe nikule mama x2*
*Oh nipe nikule mama x2*

Katika wimbo wa *Imwe munyanyae wa ili* (moja rafiki wa pili) neno *munyanyae* inayomaanisha rafiki imerudiwa ili kusisitiza ukaribu wa utaratibu unaofuatia herufi fulani baada ya nyingine.

Ukariri huu wa neno rafiki unamwezesha mtoto kufahamu ni herufi gani inakaribia lile lingine kwa haraka kuliko kama angekuwa akisomeshwa moja kwa moja; wimbo unasema:-

*Imwe munyanyae wa ili*
*Itatu munyanyae wa inya*

*Itano munyanyae wa thanthatu*

*Muonza munyanyae wa nyanya*

*kenda munyanyae wa ikumi*

*" Moja rafiki wa pili*
*Tatu rafiki wa nne*
*Tano rafiki wa sita*
*Saba rafiki wa nane*
*Tisa rafiki wa kumi"*

Wimbo wa *Syana sya nasali* pia takririri ya neno limetokea ambapo tunapata neno *ni* likirudiwa mara kadhaa. Wimbo unasema:-

*Syana sya nasali tusomei nesa*
*nitwisi kisungu yes yes no.*
*Teacher ni mwalimu*
*Chair ni kivila*
*Window ni ndilisya*
*hand ni kw'oko.*

*"Watoto wa nasari tusomeni vizuri*
*Tunajua kusoma kiingereza, yes yes, no*
*Teacher ni mwalimu*
*Chair ni kiti*
*Window ni dirisha*

*Hand ni mkono"*

Neno *ni* limetumiwa katika kusisitiza tafsiri ya neno linalotafsiriwa. Katika wimbo wa *Yesu ai kana kaseo* neno *atetheeasya* linalomaanisha alikuwa akisaidia imerudiwa. Wimbo unasema: -

*Yesu ai kana kaseo.*
*Atetheeasya asyai make*
*Atetheeasya inyia mawia*
*Kuthambya miio*
*Atetheeasya ithe Yosefu*
*Kukuna landa.*

*Yesu alikuwa mtoto mzuri, alisaidia wazazi wake*
*Alisaidia mama yake kazi ya kuosha vyombo*
*Alisaidia baba yake Josefu kupiga randa.*

Neno *atetheeasya* limerudiwa katika kusisitiza jinsi ambavyo aliweza kufanya kazi pamoja na wazazi wake katika kazi zote walizofanya, ndipo akawa mtoto mzuri mwishoni. Nia ya kurudia neno hili ni kuonyesha mtoto jinsi anavyopaswa kuwa ikiwa anataka kuwa mtoto mzuri baadaye na la muhimu ni kuwasaidia wazazi.

Mwisho katika wimbo wa *soma soma soma*, neno *wee* limerudiwa katika kila mstari. Wimbo unasema:-

*Soma soma soma wee*
*Wakati wa kusoma soma wee*
*Imba imba imba wee*
*Wakati wa kuimba imba wee*
*Cheza cheza cheza wee*
*Wakati wa kucheza cheza wee*
*Chora chora chora wee*
*Wakati wa kuchora chora wee.*

Neno hili *wee* limetumiwa hapa kama kionyeshi. Wakati wanapotaja hili, huwa wanaonyesha ni nani wanaonya juu yake, wanaweza kuonyeshana wao kwa wao ili kusisitiza dhana wanayoongea juu yake ili mtoto aweze kulitilia maanani.

Kupitia kwa takriri ambazo tumezungumzia, ni wazi kwamba takriri ilitumiwa pale ambapo pana ujumbe muhimu wa kutilia maanani.

**4.1.2 Matumizi ya Misemo**

Mbinu ya misemo huweza kufupisha ukweli na kuuweka katika maneno machache. Nyimbo za watoto wa shule za chekechea zimetumia mbinu hii kwa kiwango fulani ingawa katika hali ya kiwango duni. Katika wimbo wa *Twapenda mambo yote,* unasema:-

*Twapenda mambo yote ya shule kabisa*

*Kujua kusoma twaona furaha*
*Haa hee kuimba vyema doo*

Wanafurahia wanapojua kusoma kulingana na wimbo ingawaje wanapenda mambo yote ya shuleni. Msemo unaopigiwa mstari *twaona furaha* ndio unatoa ujumbe huu.

Msemo mwingine ambao umetumika upo katika wimbo wa *Mama nipe mayai* ambapo mtoto anamwambia mamake amechoka kunywa uji, na kwamba hakushiba anahisi njaa. Msemo *nimechoka na uji* umetumika hapa ambao unamaanisha kuwa hana haja ya kunywa uji tena kwa sababu kila siku wanakunywa uji na sasa anataka chakula cha aina nyingine. Katika kufafanua madhara ya kutumia chakula cha aina moja ambayo ni ugonjwa ndipo mtoto ataeleza maana ya msemao huu.
Wimbo unasema:-

*Mama nipe mayai nimechoka na uji*
*Ninahisi njaa*
*Kila siku ni ugali na kabeji nyeupe*
*Lazima nitapatwa na magonjwa.*

Wimbo wa *Mama yangu ameniacha* pia tumetambua matumizi ya misemo.Wimbo unasema katika kifungu ambacho msemo huu umetokea hivi:-

*Songa na mwiko mama x2*

*Oh songa na mwiko mama x2*

Msemo uliotokea hapa ni *songa na mwiko* ambao unamaanisha kitendo kinachofanywa au mtu anapopika ugali.

Matumizi ya msemo yametokea katika wimbo wa *Ethiwa wi kana ka nasali*. Wimbo unasema:-

*Ethiwa wi kana ka nasali*

*Amuka kioko tene*

*Osa kalai na savuni ukathambe*

*Tia ithau vau musyi semba vau sukulu*

*Kunua Matu withukiisye mwalimu*

*"Kama wewe ni mtoto wa nasari*

*Amka asubuhi na mapema*

*Chukua karai na sabuni ukaoge*

*Acha mchezo nyumbani*

*Kimbia hapo shuleni*

*Fungua masikio usikilize mwalimu"*

Msemo uliotumika *kunua matu* yaani kufungua masikio una maana ya kusikiliza, wimbo unashauri mtoto kuwa baada ya kuacha mchezo hapo nyumbani akifika shuleni anahitajika asikilize kile

mwalimu anamfunza. Kwa hivyo, shuleni hakuhitajiki mchezo jambo ambalo anahitajika kufanya akifika shuleni.

### 4.1.3 Matumizi Mengineyo ya Tamathali za Usemi

Matumizi ya tamathali za usemi pia yametokea katika nyimbo hizi mara moja. Katika wimbo wa maji ni maisha twatambua matumizi ya sitiara yakitokea. Wimbo unasema:-

*Maji ni maisha*
*Tunaoga nayo*
*Tunapika nayo*
*Hatuwezi kuishi bila maji*

Sitiara iliyotokea hapa ni *maji ni maisha* ambapo twaona maji yakilinganishwa na maisha kupitia kwa yale inayofanya. Twaona mwandishi akisema tunaoga na kupika nayo na kwamba bila maji hatuwezi kuishi, jambo ambalo ni la kweli.

Tukikosa kuoga na kula kwa kweli hatuwezi kuishi na ndipo imelinganishwa na maisha.
Katika wimbo wa *Imwe munyanyae wa ili* pia twatambua matumizi ya tamathali ya usemi ambapo wimbo unasema:-

*Imwe munyanyae wa ili*
*Itatu munyanyae wa inya*
*Itano munyanyae wa thanthatu*

*Muonza munyanyae wa nyanya*

*Kenda munyanyae wa ikumi*

Hapa twaona tashhisi ikitokea ambayo ni *Munyanyae* inayomaanisha rafiki ambapo nambari za kuhesabu zalinganishwa kwa kutumia neno rafiki. Nia ya kutumia neno hili nikumwezesha mtoto kufahamu kwa urahisi utaratibu wa kuhesabu au kufuatanisha herufi za kuhesabu.

**Hitimisho**

Katika sehemu hii tumebainisha ambavyo jinsi tamathali mbali mbali zimetokea katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Baadhi ya zile ambazo zimetokea ni kama vile takriri ambazo tumeona kuwa zinatawala nyimbo hizi na matumizi ya misemo. Pia taswira na tashhishi zimetokezea katika nyimbo hizi ingawa kwa kiwango kidogo sana.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunashughulikia matokeao ya utafiti wetu wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Moja na matatizo yaliyotukumba wakati wa kufanya utafiti huu. Tumetamatisha kwa kutoa mapendekezo ya tafiti zingine ambazo zinaweza kufanywa kuhusu uwanja huu tulioushughulikia.

## 5.1 Eneo la Kazi kwa Jumla

Utafiti huu umejihusisha na uchanganuzi wa matendo katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea katika kuwasilisha nyimbo. Tulishughulikia nyimbo kumi na tano katika viwango vifuatavyo:

a) Maudhui
b) Sentensi
c) Msamiati ulioteuliwa
d) Tamathali za usemi

Sura ya kwanza ya kazi hii imezungumzia mada ambayo tumefanyia utafiti wetu. Katika kushughulikia swala hili, tumeanza kwa kujadili swala la utafiti na kuendelezea kusudi letu la kufanya utafiti huu. Pia, tumeelezea sababu za kuteua swala letu, sababu za



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kuteua nyimbo za watoto wa shule za chekechea na upeo wa kazi yetu.

Sura ya pili imejadili historia ya fasihi nchini Kenya pamoja na sifabia za fasihi ya watoto. Umuhimu wa kuangalia sehemu hizi mbili ni kutoa mwangaza kwa kazi iliyokuwa inatafitiwa. Hii ni kwa sababu fasihi ya watoto haijaingiliwa sana na watafiti mbali mbali jambo ambalo lilifaa sana na kudokezea historia kwa wasomaji na watafiti wa baadaye. Katika kufanya haya sura hii iligawanywa katika sehemu mbili ambazo ni:-

(i) Historia na maendeleo ya fasihi ya watoto nchini Kenya.

(ii) Sifabia ya fasihi ya watoto.

Katika sehemu ya kwanza inayohusu historia ya watoto, vipindi vitatu vimeshughulikiwa ambavyo ni:-

(i) Kipindi cha kabla ya ukoloni

(ii) Kipindi cha ukoloni

(ii) Kipindi cha baada ya ukoloni.

Katika sehemu ya pili ambayo inahusu sifabia ya fasihi ya watoto tulishughulikia vipengele vinne ambavyo ni:-

(i) Maana ya fasihi ya watoto

(ii) Dhima ya fasihi ya watoto

(iii) Sifabia za fasihi ya watoto

(iv) Uteuzi wa fasihi ya watoto.

Katika sura ya tatu tumejadili maudhui ambayo yanatokea katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Nyimbo zote ziliweza kushughulikia maudhui mbalimbali ingawa yale ya kielimu ndiyo yaliyojitokeza kwa kiasi kikubwa.

Tulipozichanganua, tuligundua ya kwamba nyimbo za kufunza watoto juu ya kuhesabu nambari za hesabu pamoja na zile zimetokea.

Katika kufanya hivi, watoto waliweza kuzikariri kwa kuimba. Kulingana na nyimbo hizi, tumetambua ya kwamba herufi hizi ndizo msingi wa elimu ya yote yule na kwa hivyo mtoto anahitajika kufahamu kuzitamka na kuzihesabu, pia kupitia kwa nyimbo hizi za watoto wa chekechea, tumegundua ya kwamba watoto waliweza kufunzwa jinsi ya kutafsiri maneno Kikamba kwa Kiingereza.

Imedhihirika kwamba hali hii inamwekea msingi mtoto katika elimu yake kama vile tuliona nyimbo hizi zaenda sambasamba na silabasi ya elimu ya watoto hawa.

Maudhui mengine ambayo yamejadiliwa katika nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea ni yale ya umuhimu wa mama kwa mtoto. Katika kujajadili, yanadhihirisha kwamba mama ni muhimu sana katika maisha ya mtoto. Katika upande wa kumtafutia chakula

na hata kumlisha mama ameonyeshwa kuwa bila yeye, mtoto hawezi akala kwa sababu ndiye anayempikia na hata kumlisha.

Hata twaona mama akiwasilishwa katika nyimbo hizi kama mwenye kujua lishe bora. Pia twatambua maudhui mengine yaliyotokea katika nyimbo hizi kama vile ya maji yanayodhihirisha jinsi maji yalivyo muhimu katika maisha ya mwanadamu. Yanaonyesha kwamba bila maji maisha hayawezi yakaendelea. Twayatumia kwa kuoga na kupika. Tumetambua nyimbo zinazotoa maudhui ya taifa letu pia ambayo yanadhihirisha jinsi watu wanavyohitajika kuungana hata kama wako katika vyama tofauti. Watu wakiwa na umoja kulingana na nyimbo hizi kutakuwa na maendeleo. Maudhui haya yanafungua akili za watoto kwamba wajione wao wakiwa kitu kimoja hata watakapokuwa watu wazima.

Maudhui haya yanafungua akili za watoto kwamba wajione wao wakiwa kitu kimoja hata watakapokuwa watu wazima.

Maudhui mengine ambayo yamezungumziwa na nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea ni yale ya ushauri. Tabia kama vile kutosoma inafanya mtu kutaabika maishani huweza kukosa heshima na kuwa na tabia ya kutangatanga huku na kule wakitafuta chakula. Tabia kama hii ya kutosoma yahitajika kukomeshwa kabisa.

Sura ya tatu pia imejadili aina ya sentensi zilizotumika katika nyimbo hizi za watoto wa shule za chekechea. Katika uchambuzi wetu tumetambua ya kwamba sentensi tofauti tofauti zimetumiwa katika nyimbo hizi kwa malengo maalum. Sentensi ndefu zilitumika wakati wa maelezo jambo ambalo linadhihirika mahali ambapo kisa fulani kinahadithiwa. Matumizi ya sentensi fupi fupi yamedhihirika katika nyimbo hizi mahali ambapo zimetokea katika kibwagizo cha wimbo au mahali sentensi inakaririwa kwa mara fulani katika wimbo. Uchovu unaotokana na sentensi ndefu wa kurudia ndio umefanya sentensi fupi fupi zitumike katika mahali kuna kukariri kwa sentensi hizi au kibwagizo.

Tunatambua kwamba kuna matumizi ya sentensi zilizotongolewa katika nyimbo hizi. Hapa, wavulana ndio hutumika katika kutongoa sentensi hizi. Sentensi hizi huweza kupitisha ujumbe wa ziada ambao hawangeweza kuingiza katika mfululizo wa mambo. Ilibainika kuwa sentensi hizi zilitumiwa kuleta uhai katika wimbo kwa kuwa baada ya sentensi hii iliyotongolewa kutajwa, waliweza kucheka.

Katika upande wa matumizi ya msamiati, imebainika kwamba uteuzi wa maneno katika nyimbo hizi haukuwa wa kiwango cha juu. Maneno ya kawaida yaliweza kutumika kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya kuwezesha watoto kufahamu ujumbe unaotokea katika nyimbo hizi. Jambo hili linadhihirisha ukweli kwamba

uteuzi wa maneno unafanywa kulingana na hadhira lengwa, maudhui na hata kipindi ambacho wimbo ulitungwa.

Katika uchambuzi wetu, tumetambua matumizi ya kuchanganya ndimi na tena matumizi ya misimu yanayotumiwa kudhihirisha hali ya kujitambulisha kwa wasikilizaji waliolengwa na mwimbaji kama vile Wambua (2001) anavyosema. Anasema kuwa matumizi ya maneno ya lugha tofauti na ile iliyotumiwa kutungia wimbo yanaonyesha kwamba mapokezi ya wimbo hutegemea mazingira na pia yaonyesha kuwa kila wimbo ulikuwa umelenga wasikilizaji maalum. Anaendelea kusema kuwa nyimbo ambazo zimelenga vijana ndizo ambazo zinatumia kauli hii kuchanganya ndimi kwingi na hata kufikia kiwango cha kutumia "sheng" ambayo ni lugha ya vijana.

Katika sura ya nne tumechanganua tamathali za usemi katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Tumeangalia jinsi ya matumizi ya tamathali hizo. Ingawa kulingana na utafiti huu imedhihirika kwamba kama vile tulivyotambua kwamba matumizi ya msamiati ni ya kiwango cha chini, hata hivyo jambo hili limetokea katika upande wa tamathali za usemi. Tamathali za usemi zilizotumiwa hapa tumegundua kwamba mwandishi alizitumia ili aonyeshe kuzifahamu na pia kutaka kuwasiliana kwa njia ya kisanaa. Pia msanii aliweza kuunda tamathali za usemi ambazo ziliweza kutoa maana kwa mwimbaji na hata msikilizaji.

## 5.2 Matatizo na Mafanikio Tuliyokumbana nayo

Katika kazi yetu ya utafiti, tulikusudia kuchanganua nyimbo za watoto wa shule za chekechea kimtindo. Haja yetu ya utafiti huu ilikuwa kuangalia kama inawezekana vipengele vinavyounda mtindo kutumiwa kutathmini nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Baaada ya kufanya haya, tumeweza kufanikiwa na kutambua kuwa nyimbo za watoto wa shule za chekechea zinaweza kuwa na mtindo wa kipekee kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi.

Pia tumefanikiwa kuonyesha kuwa nyimbo hizi zaweza kutumiwa kufunzia lugha na maudhui kama ilivyo katika tanzu zingine za kifasihi. Kwa hivyo waalimu wa shule hizi za watoto wa chekechea wanahitajika kuzitilia maanani kwa sababu zina athari kubwa kwa watoto hawa hasa katika upande wa lugha na maudhui.

Kwa upande mwingine, tuliweza kutatizika katika kazi yetu kutokana na kutokuwepo kwa vipengele hivi moja kwa moja. Ilichukua muda kutofautisha tamathali ya usemi na msamiati wa kipekee. Pia nyimbo za Kikamba ziliweza kututatiza wakati wa kuzitafsiri kwa sababu dhana zingine zipo katika lugha ya Kikamba lakini hazipo katika lugha ya Kiswahili. Wakati wa kuzitafsiri ilikuwa ni rahisi kupoteza maana ya dhana hiyo.

Pia tuliweza kupata tatizo wakati wa kunasa nyimbo hizi; watoto hawangeweza kuwa watulivu wakati wa kuimba hadi mwisho. Hii

ni kwa sababu watoto hawa hawakuwa wa umri mmoja; wengine walikuwa wachanga zaidi kuliko wengine. Waliweza kuanza kucheza katikati ya wimbo unaonaswa na hivyo kutufanya kurudia mara kadhaa.

### 5.3 Mapendekezo kwa Utafiti zaidi

Utafiti umejihusisha na mtindo katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Tumeangalia jinsi lugha na tamathali za usemi zilivyotumika katika kuwasilisha maudhui au ujumbe. Kwa hivyo, hatukuingilia maudhui kwa undani kwa sababu haja yetu katika utafiti huu ilikuwa ni kuangalia jinsi lugha ilivyotumika pamoja na kuchambua aina za tamathali zilizotumika katika nyimbo hizi. Kwa hivyo, ndiyo sababu tumeingilia kwa undani matumizi ya lugha katika nyimbo hizi.

Ni wazi kwamba kuna mambo mengi ambayo hatukuyashughulikia na ambayo yeyote aliye na hamu ya kufanya utafiti zaidi kuhusu nyimbo hizi anaweza kuchunguza. Hivyo basi ni mapendekezo yetu tafiti zingine zifanywe katika mada zifuatazo:-

(i) Utafiti unaweza kufanywa kwa kuchunguza umuhimu wa maudhui yanayowasilishwa na nyimbo hizi kwa mtoto. Utafiti kama huu utabainisha ni kwa kiasi gani maudhui haya yanabadilisha mtoto kulingana na lengo la wimbo ulioimbwa.

(ii) Utafiti ufanywe kuhusu matumizi ya lugha katika nyimbo za lugha zingine kama vile Kiluo, Kiluhya au Kikuyu. Hii ni kwa sababu utafiti wetu ulishughulikia nyimbo za Kikamba na Kiswahili pekee. Umuhimu wa utafiti kama huu utaweza kubainisha kama nyimbo hizi zina ulinganifu au sifa sawa. Hapo mtafiti ataweza kutoa sababu za tofauti hizi.

(iii) Pia tungependelea utafiti ufanywe kuhusu uhusiano uliopo baina ya nyimbo za watoto wa shule za chekechea na za wale wa umri wa juu. Hapa mtafiti atahitajika kuangalia uhusiano wa maudhui, matumizi ya lugha na hata tamathali za usemi. Pia ataweza kuchunguza uhusiano wa kuziwasilisha ambapo ataangalia muundo na mbinu mbalimbali za kuwasilisha nyimbo hizi.

(iv) Vile vile tumetoa mapendekezo utafiti ufanywe kuhusu maudhui katika nyimbo za watoto wa shule za chekechea. Pendekezo hili latokana na wazo kwamba nyimbo hizi hutungwa kulingana na silabasi ya shule za chekechea.

(v) Kwa kuhitimisha, utafiti unaweza pia kufanywa kuhusu ulinganifu uliopo baina ya sifabia za nyimbo za watoto wa shule za chekechea na zile shule za umri wa juu. Pendekezo hili litatoa mpaka kati ya nyimbo za watoto

hawa na wale wa kiwango cha juu kwa sababu kuna uwezekano wa mwingiliano wa nyimbo hizi.

**Marejeleo**

Akivaga. S.K. na A.B Odaga (1982). *Oral Literature A School Certificate Course.* Nairobi: Heinemann.

Akoleit. J. (1990) . "Response and Criticism in Children's Literature in Kenya: The case of Barbar Kimenye": M.A Thesis (unpublished) Kenyatta University.

Bowman. W.D. (1998). *Philosophical Perspective on Music.* London: Oxford University Press.

Chiuri. J. (1984). " Pop Music as a form or oral Literature: A survey of Joseph Kamaru" (Tasnifu ya PGDE- Chuo Kikuu cha Nairobi).

Coombes. H.(1953).*Literature and Criticism.* Chatto & Windus: Harmondsworth

Crystal. D. na Davy (1969). *Investigating English style.* London: Longman.

Finnegan. R. (1970). *Oral Lliterature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Gituku. A.N (1990). "Maigizo ya Kienyeji ya Watoto Nchini Kenya Nafasi ya kuyatumia katika ufundishaji". Tasinifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kamau. M. (1994). "Ufundi katika Riwaya za Mohammed Said Abdalla". Tasnifu ya M. A Chuo kikuu cha Kenyatta.

Kieti. M. na P. Coughlin (1990). *Barking, you will be eaten! The wisdom of Kamba Oral Literature.* Nairobi: Phoenix

King'ei. G. (1990). "Culture and Communication: The role of Swahili Taarabu Songs in Kenya from 1963-1990". Unpublished Ph.D. Dissertation, Harvard University, America.

King'ei. G.K. na Kisovi. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kirumbi. P. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi.* Shugwaya Publishers.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Leech. G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry.* London: Longman.

Mazrui. A.M. na Syambo. B.K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Miruka. O. (1994). *Encounters with Oral Literature.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohammed. S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili.* Nairobi: E.A P H.

Mpesha. G.N (1995). "Children's Literature in Tanzania Literary Appreciatation of its Growth and Development". Unpublished PHD Thesis. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mugambi P. (1982). "Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Ki -Kenya zilizochapishwa". Tasnifu ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mulokozi. (1989). *Tanzu za fasihi-* Mulika 21. Dar-es-alaaam: Tuki.

Mutwiri. G. (2005). "Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso katika Jamii ya Watingania". M.A. Thesis Kenyatta university.

Nandwa. J. and Bukenya, A. ( 1983). *African Oral Literature for Schools.* Nairobi: Longman.

Ngara. E. (1981). *Stylistic Criticism and the African Novel.* London: Heinemann.

Ngure. A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa shule za Sekondari.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu. K & Rocha. C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkonge. K. (1988). " A Literary Study of the Songs of Joseph Kamaru Themes and Style". B.Ed project. Kenyatta University.

Ntarangwi. M. (1990). " Uhakiki wa Maudhui ya Utetezi katika Utunzi wa Remmy Ongala". M.A. Thesis. Kenyatta University.

Odaga. A.B. (1980). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: K.K.B.

Okhoba. E. W. (1985). "Style and Meaning of Abamarachi Children's Oral Poetry". M.A. Kenyatta University.

Osore. K. M. (1994). "Uhakiki wa Kiisimu wa Riwaya za Suleiman Mohamed". (Tasnifu ya M.A- Chuo Kikuu cha Kenyatta).

P. Bitek. Okot. (1973). *African's Cultural Revolution..* Nairobi: Macmillan.

Ruo Kimani Ruo (1989). *Nguzo za ushairi wa Kiswahili.* Nairobi: Macmillan Kenya.

Tuki. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu..* Nairobi: Oxford University Press.

Wambua. S. (2001). " Mtiondo katika Nyimbo za Kakai Kilonzo". M.A. Thesis, Kenyatta University.

Wamitila K.M. (2002). Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila K. M. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publication

Weche. (2002). "Children's Literature. An image forming force: Case Study of Ezekiel Alembi's Books". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**Kiambatisho cha Kwanza: Hojaji kwa Walimu wa Shule za Chekechea.**

Jina______________________________Jinsia: Mke ☐ Mume ☐

**Umri:**

Kati ya miaka-:

a. 15-25 ☐

b. 25-35 ☐

c. 35-45 ☐

d. Zaidi a miaka 45 ☐

**Kiwango cha Elimu:**

a. Chini ya darasa la nane (Kiwango cha chini) ☐

b. Kati ya kidato cha kwanza hadi cha nne (Kiwango cha kati) ☐

c. Juu ya kidato cha nne (Kiwango cha juu) ☐

**Mahali unapoishi** __________________________________________

**Swali la Kwanza:**

Ulianza kufunza shule za chekechea lini?

..................................................

..................................................

**Swali la Pili:**

Umefunza shule ngapi tangu ulipoanza kufundisha shule hizi?

..................................................

..................................................

**Swali la Tatu:**

Ni nini kilichokufanya uanze kufundisha shule hizi?

..................................................

..................................................

**Swali la Nne:**

Unapenda kufundisha watoto hawa? Kwa nini?

..................................................

..................................................

**Swali la Tano:**

Watoto wa shule za chekechea huwa na umri ngani?

..................................................

..................................................

**Swali la Sita:**

Kulingana na umri wao, kuna shida unazopata unapowafunza nyimbo?

..................................................

..................................................

**Swali la Saba:**

Nyimbo wanazoimba hutegemea nini?

..................................................

..................................................

**Swali la Nane:**

Nyimbo hizi zinatungwa na nani?

...................................................

...................................................

**Swali la Tisa:**

Wanapenda kuimba aina zote za nyimbo mnazowafunza?

...................................................

...................................................

**Swali la Kumi:**

Ni aina zipi za nyimbo mnazoimba shuleni?

...................................................

...................................................

**Swali la Kumi na Moja:**

Mnaimba na wao wanapoimba au la?

...................................................

...................................................

**Swali la Kumi na Mbili:**

Katika utunzi wenu, tanakali za usemi mlizotumia zilitokana na mipango au zilitokea kiajali?

...................................................

...................................................

**Swali la Kumi naTatu:**

Mnanyimbo ambazo hazikutumia tamathali za usemi? Kwa nini?

...................................................

..................................................

**Swali la Kumi na Nne:**

Unafikiri kupitia kwa maoni yako matumizi yenu ya lugha yalifaidi jamii kwa njia zipi?

...................................................

..................................................

**Swali la Kumi naTano:**

Tukilinganisha na nyimbo zile zingine ni nini hasa kinachoweza kuchukuliwa kama upekee wa mtindo wenu?

..................................................

..................................................



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Kiambatisho cha Pili: Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea.**

**Nyimbo zilizochanganuliwa**

1. **Twapenda mambo yote**

Twapenda mambo yote ya shule kabisa
Kujua kusoma twaona furaha
Haa hee kuimba vyema doo

2. **Mama yangu ameniacha**

Mama yangu ameniacha
Akaenda zake kwa wazazi
Sina mtu hata mmoja
Wakunipatia chakula
Tiririri mama x2
Oh tiririri mamax2
Pika chakula mama x2
Oh pika chakula x2
Songa na mwiko mamax2
Nipe nikule mamax2
Tiririri mamax2
Oh tiririri mamax2

**3. Mama nipe mayai**

Mama nipe mayai
Nimechoka na uji
Ninasikia njaa
Kila siku ni ugali na kabeji nyeupe
Lazima nitapatwa na magonjwa
Nyama, boga, mahindi, maziwa na matunda
Tukitumia tutapata nguvu
Kazi zetu twafanya na kucheza twacheza
Twaruka hivi hivi na furaha

**4. Andu ala matasomaa**

Andu ala matasomaa mathinaa muno
Maitinda maitangatanga maimantha kya kuya
Utuku wavika maitula mbemba syeene
Andu tasu ti ma ndaia.
Andu!

*Watu wale hawasomi hutaabika sana*
*Hushinda wakitangatanga wakitafuta cha kula*
*Usiku ukifika wanakata mahindi ya wenyewe*
*Watu kama hao sio waheshima.*
*watu!.*

**5 Maji ni maisha**

Maji ni maisha

Tunaoga nayo

Tunapika nayo

Hatuwezi kuishi bila maji

**6 Taifa lenye nguvu**

Taifa lenye nguvu ni taifa ambalo watu wake wameungana

Uwe mwana KANU

Uu KANU

Uwe mwana FORD

Uu FORD

Uwe mwana DP

Uu DP

Uu uu tuungane tujenge taifa lenye nguvu

Watoto wa Kenya

Sisi tunataka taifa moja.

**7. Nyumba ni nzeo**

Nyumba ni nzeo

Miomo, Ndilisya, vamwe na kiala, mokuta na miti ila

mivande nza

Nyumba ni nzeo

Nyumba ya musyi

Nivo kila mundu wivithaa

*Nyumba ni nzuri*

*Nyumba ya kuishi*

*Milango, dirisha, pamoja na paa, kuta na miti*

*iliyopandwa nje*

*Nyumba ni nzuri*

*Nyumba ya kuishi*

*Ndipo kila mtu hujificha.*

**8. A, e, i, o,u**

A, e, i, o,u

Hizi ni herufi tu

Toka kwa sauti tu

Hizi a,e,i,o, u

A- Angalia

E – Enda

I- Ingia

O-Ondoka

U-Usiende.

**9. Watoto wema**

Watoto wema njooni tusome
Sikiliza kengele
Ding, dong ding

**10. Mundu utesi kuthamba**

Mundu utesi kuthamba ni ndia yi kithingo
Kuthamba ni kuseo
Tusuaniei kuthamba
Ngaamuka ngathamba mwii
Nzanue nzwii
Na ndyela mbwaa
Nikana nithiwe nimutheu
Kw'u kw'u kw'u

*Mtu asiyejua kuoga ni mjinga kabisa*
*Kuoga ni kuzuri tufikirie kuoga*
*Naamka asubuhi*
*Ninaoga mwili*
*Ninachana nywele na kukata kucha ili niwe msafi*
*Kabisa kabisa kabisa*

**11. Syana sya nasali**

Syana sya nasali tusomei nesa
Nitwisi kisungu *yes yes no*
*Teacher* ni mwalimu
*Chair* ni kivila,
*Window* ni ndilisya,
*Hand* ni kw'oko

*Watoto wa nasari tusomeni vizuri*
*Tunajua kusoma Kiingereza,* yes yes, no
Teacher *ni mwalimu*
Chair *ni kiti*
Window *ni dirisha*
Hand *ni mkono*

**12. Ethiwa wi Kana ka Nasali**

Ethiwa wi kana ka nasali
Amuka kioko tene
Osa kalai na savuni ukathambe
Tia ithau vau musyi semba vau sukulu
Kunua matu withukiisye mwalimu

*Kama wewe ni mtoto wa nasari*

*Amka asubuhi na mapema*

*Chukua beseni na sabuni ukaoge*

*Acha mchezo nyumbani*

*Kimbia hapo shuleni*

*Fungua masikio usikilize mwalimu*

**13. Imwe munyanyae**

Imwe munyanyae wa ili

Itatu munyanyae wa inya

Itano munyanyae wa thanthatu

Muonza munyanyae wa nyanya

Keenda munyanyae wa ikumi

*Moja rafiki ya pili*

*Tatu rafiki ya nne*

*Tano rafiki ya Sita*

*Saba rafiki ya nane*

*Tisa rafiki ya kumi*

**14. Yesu ai kana kaseo**

Yesu ai kana kaseo

Atetheeasya asyai make

Atetheeasya inya mawia

Kuthambya miio

Atetheeasya ithe Yosefu

Kukuna landa

*Yesu alikuwa mtoto mzuri*

*Alisaidia wazazi wake*

*Alisaidia mama yake*

*Kazi ya kuosha vyombo*

*Alisaidia baba yake, Josefu*

*Kupiga randa*

**15. Soma soma soma**

Soma soma soma wee x2

Wakati wa kusoma soma wee

Imba imba imba wee x2

Wakati wa kuimba imba wee

Cheza cheza cheza wee x2

Wakati wa kucheza cheza wee

Chora chora chora wee x2

Wakati wa kuchora chora wee.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY